Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 82 No. 229 | JAM.II-RAJAB.1443 AH | MARCH 2022 | TABLIGH 1401 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Na aliposema Isa bin Mariamu: Enyi wana wa Israeli, mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu, nisadikishaye yaliyo mbele yangu katika Taurati na ku- toa habari njema ya Mtume atakayefika nyuma yangu jina lake ni Ahmad; lakini alipowafikia kwa Ishara zilizo wazi, wakasema: Huu ni udanganyifu dhahiri

Alhamdulilaih!!

AHMADIYYA YATIMIZA MIAKA 133

(1889 - 2022)



Hazrat Mirza Ghulam Ahmad

Mwanzilishi wa Ahmadiya - 1889

Na Mwandishi wetu

Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya ilianzishwa kwa amri ya Allah mwaka 1889 na Hazrat Mirza Ghulam Ahmad aliyedai kuwa Masih na Mahadi sawa na bishara iliyotolewa na Mtukufu mtume Mohamad[saw]. kazi iliyotumwa na Allah kuifanya na amabayo imekwisha fika zaidi ya nchi 120 duniani ni kumrejesha binadamu kwa mola wake na kumuelimisha binadamu juu ya wajibu wake kwa Allah na viumbe wake.

Ni jumiayahii pekee duniani ambayo kwa kufuata nyayo za Mtume Mtukufu [saw] inaendeleza nidhamu ya Ukhalifa ulionza mwaka 1908 alipofariki masih aliyeahidiwa na kuchaguliwa Hazrat Hakim Noordin[ra] kuwa Khalifatul Masih wa kwanza aliyefuatiwa na Khalifatul Masih wa pili Hazrat Mizah Bashir-u-din Mahmood Ahmad[ra] , Khalif atul wa watatu Hazrat Mirza Nasir Ahamad [rha],

Inaendelea uk. 4

MAPENZI YA SEYDNA AHMAD KWA MTUME S.A.W.

Allah Subhanahu wa Taalah anasema ndani ya Kurani Tukufu

قُلْ إِن كانَ آباؤُكُم وَأَبناؤُكُم وَإِخوانُكُم وَأَزواجُكُم وَعَشيرَتُكُم وَأَموالٌ اقتَرَفتُموها وَتِجارَةٌ تَخشَونَ كَسادَها وَمَساكِنُ تَرضَونَها أَحَبَّ إِلَيكُم مِنَ اللَّهِ وَرَسولِهِ وَجِهادٍ في سَبيلِهِ فَتَرَبَّصوا حَتّى يَأتِيَ اللَّهُ بِأَمرِهِ وَاللَّهُ لا يَهدِي القَومَ الفاسِقين- [٩:٢٤]

(Sheikh Karim Uddin Shams. Mbeya)

Tafsiri: Sema, kama baba zenu, na wana wenu, na ndugu zenu, na wake zenu, na jamaa zenu, na mali mlizochuma, na biashara mnazoogopa kusimama, na majumba mnayoyapenda ni vipenzi Zaidi kwenu kuliko Allah na Mtume Wake na kufanya juhudi katika njia Yake, basi ngojeni mpaka Allah Alete amri Yake, na Allah Hawaongozi watu waasi.

Ukweli ndio huu kwamba, upendo wa seyyedna Ahmad as. kwa Bwana wake ulikuwa kiini cha roho yake na uzima wake, matukio mbali mbali, yapendezayo yaliyojaa mapenzi, mahaba na utii usio wa kwaida, yanaonekana maishani mwake kiasi hiki kwamba mtu anapigwa na bumbuwazi.

Masharti na vigezo vyote vya mapenzi ya kweli vina hakiki katika kila secunde ya maisha yake, ambayo yananga'a na mifano ya aina hii kama mbingu inavyonga'a kwa nyota mbali mbali. Naweza kusema kwa haki kwamba jinsi Seyidna Ahmad a.s. alivyompenda Mtume (s.a.w.) kakuna mwingine awezaye kujifananisha naye, wala upendo wake kwa Mtume (s.a.w) haune mfano katika historia yote ya Kiislam. Mtu yoyote hawezi kupinga kauli hii kuwa: daraja na makamu ya Seyidna Ahmad a.s. katika kumpenda Mtume (s.a.w) iko juu zaidi hata kuliko akili na fahamu ya watu.

Inaendelea uk. 10

بسم الله الرحمٰن الرحيم

MUHTSARI WA HOTUBA YA IJUMAA ILIYOTOLEWA NA HADHRAT AMIR UL MOMENIN, KHALIFAT UL MASIH V ATBA -(KATIKA MASJID MUBARAK, ISLAMABAD (UK), TAREHE 04/02/2022

Makhalifa Waongofu – Hazrat Abu Bakr (ra)

Baada ya Tashahhud, Ta'awwudh na Surat Faatihah, Hadhrat Khalifatul Masih V, Hadhrat Amir ul Momeniin, Mirza Masroor Ahmad atba ('Ayyadahullahu Ta'ala Bi-Nasrihil Aziiz'); alisema kuwa, ataendelea kuangazia matukio kutoka katika maisha ya Hadhrat Abu Bakr (r.a):

Inaendelea uk. 3

IMANI NA UTUMIAJI WA AKILI

Dr Kitabu Pazi

Kwa kawaida mwanadamu hupata habari kupitia vyanzo vikuu viwili kuona au kisikia na Akili hufanya upembuzi yakinifu ili kupata uhakika wa jambo husika, na Jambo hilo likikosekana uhakika akili hulikataa na mwanadamu hawezi kulikubali.

Na mungu ndivyo anavyotaka mtu atumie kipawa alicho pewa (AKILI) kutafakari mambo na usipofanya hivyo anasikitika sana.

Watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa;

Inaendelea uk. 5

Mahubiri katika mji wa Bagamoyo UK 4

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

WAJIBU WETU

Kazi aliyonayo kila Mwislamu wa kweli na mwenye uchungu duniani ni kutafuta kwa udi na uvumba masingizio dhidi ya Mtukufu Mtume saw popote yanapojitokeza na hivyo kuyafuta masingizio hayo kwa hoja na kuweka taswira iliyosahihi na yenye Ushahidi wa kihistoria. Kama kuna binadamu aliyeonewa na kufanyiwa dhuruma kubwa basi ni Mtukufu Mtume Saw. Masinghizio hayo kwa masikitiko makubwa yanakwenda kwa yule aliyetupenda sote binadamu bila ubaguzi na Allah akamtangaza ya kwamba ni *Rehmatul* alamiin kwa viumbe wake wote. Kumsingizia kiumbe mwema wa namna hii ni uonevu uliopitiliza mipaka. Utamgusaje binadamu yule ambaye hata kinda wa ndege alimuonea huruma na akawaambia Mashaba wamrudishe kwa mama yake? Utangusaje yule ambaye mateso yote aliyoyapata mjini Makka na aliporudi wakati wa ushindi akawasamehee wote kama Nabii Yusuph[as] alivyowasamehe ndugu zake.

Lakini kama wasemavyo waswahili akutukanaye hakuchagulii tusi. Hata wanahistoria mahili kama Profesa William Muir naye amedumbukia katika shimo hilo la husda na inda. Unawezaje na ujasiri huu unautoa wapi wa kumsingia Mtume Saw katika ndoa zake? Wao wanasema na Allah apishe mbali kwamba ndoa zilisukumwa na matamanio yake ya kimwili. Ni masingio na uonevu mkubwa. Kabla ya kutangazwa kuwa Mtume mji wote wa Makka ulikuwa shahidi juu ya usafi wake na uaminifu. Hakuna doa lolote linalonasibishwa na tabia yake. Akiwa na miaka ishirini na tano alimuoa Mama mwenye umri wa miaka arobaini je hiyo ni alama ya matamanio? Toka miaka ishirini na tano hadi Bi Khadija r.a anafariki Mtukufu Mtume [saw] hakuoa mke mwingine. Akiwa na miaka hamsini na tano alimuoa Bi Sauda r.a ambaye umri wake ulikuwa umekwenda na alikuwa mjane. Wazee wa Makka walisumbuka sana na kasi ya mafundisho ya Mtukufu Mtume saw juu ya mahubiri na hivyo wakapanga mbinu waliyodhani watamtoa kwenye mstari. Walimwambia ya kwamba ukiacha kutukana masanamu yao watampa Binti yoyoyte unayemtaka. Sikiliza majibu yake hata mchukue jua mliweke mkono wa kulia na mwezi mkono wa kushoto. siwezi kuacha kutangaza umoja wa Allah. Ni aibu kubwa kwa wale ambao ni bingwa wa kusingizia.

Historia imeweka bayana kuwa usiku alikuwa akiamka na kusali tahajjudi hadi miguu inavimba na huyo ndiye anayesingiwa na masingizio hayo yasokichwa wala miguu.

Ukizingatia yote hayo utauona umuhimu wa kila mwislamu kutafuta shutma dhidi ya Mtukufu Mtume[saw] na kutoa maelezo yanakwenda sawa na Kurani Tukufu, Sunna na Hadithi. Kazi tukufu ya kung'arisha kuweka bayana utukufu wa mtume saw si kazi ndogo. Upande wa pili wamejipanga kwa hali na mali kufanikisha azima yao. Sisi pia tunahitaji silaha zifuatazo ili kushinda vita hii. Uchamungu, Elimu, Mikakati na haya yote hayapatikani isipokuwa kupitia kwa Khalifa ambaye ni muwakilishi wa Allah aridhini. Tusijidanganye hata kidogo kwamba tunaiweza kazi hii bila ya Khalifa.

Ni neema kubwa iliyoje kwamba kwa hivi leo ni jumuiya pekee duniani ilio na Khalifa. Kazi yake kubwa ni kuwakumbusha binadamu juu ya wajibu wao kwa Mola pia kwa viumbe wa Allah. Na kazi hii inaweza kufanikiwa wakati mnae kiongozi ambaye mnamtii. Bila utii kwa kiongozi hakuna mafanikio. Wakati tunashughurika katika kulinda na kutetea heshima ya mtukufu Mtume[saw] roho zetu na fikra zetu na mawazo yetu vyote hivi viende kwa vita Uhudi. Katika vita vita ya Uhudi kuna somo kubwa na pana la utii. Kiongozi tuliyenae ni kwa kiasi gani tunatii na kutekeleza yale anayotwambia? Kushindwa kwetu na kufaulu kwetu kutategemea utii tunauonesha kwa kiongozi, tusikilize anayotwambia na tutekeleze.

Tueleze kidogo juu ya vita ya Uhudi. Mtukufu mtume saw aliwaambia maswahaba kwamba ameona katika njozi wakipigana na maadui hapo hapo walipo. Vijana kwa jazba zao wakashauri wawafuate maadui walipo kwenye mlima uhudi. Pia mtume saw alisisitiza sana tena sana ya kwamba hata mkiona ya kwamba tumeshinda katukatu msitoke juu ya mlima. Yaliyotokea ni historia. Waislamu ambao walishapata ushindi walipata mtikisiko mkubwa. Hata Ghazwal zilizofuata ni kule kujitutumua kwa yale yaliyotokea uhudi.

Kazi ya kulinda heshima ya Mtume[saw] ni kubwa na maadui wanaongozeka kila kukicha. Bila kiongozi, bila ukhalifa kazi hii itakuwa ngumu. Ushindi utatokana na kusikiliza na kufuata anayotuamulisha Khalifatul Masihi. (atba) Mara kwa mara anatoa miongozo na bilhususi siku hizi kupitia MTA tujenge utamaduni wa kuwa karibu na MTA. Ni sauti ya Khalifa kama ilivyokuwa sauti ya Sayyidina Omari r.a ya kuwaonesha askari wa kiislamu adui alipo. Ni sauti ya Huzur inayotambua adui alipo



QUR'AN TUKUFU

Sura Aal-Imran : 55

إِذْ قَالَ اللَّهُ يَا عِيسَىٰ إِنِّي مُتَوَفِّيكَ وَرَافِعُكَ إِلَيَّ وَمُطَهِّرُكَ مِنَ الَّذِينَ كَفَرُوا وَجَاعِلُ الَّذِينَ اتَّبَعُوكَ فَوْقَ الَّذِينَ كَفَرُوا إِلَىٰ يَوْمِ الْقِيَامَةِ ۖ ثُمَّ إِلَيَّ مَرْجِعُكُمْ فَأَحْكُمُ بَيْنَكُمْ فِيمَا كُنتُمْ فِيهِ تَخْتَلِفُونَ

(Kumbukeni) Allah aliposema: Ewe Isa! kwa yakini Mimi Ndiye Mwenye kukufisha, na kukuinua kwangu, na Nitakutakasa na (masingizio ya) wale waliokufuru, na nitawaweka wale waliokufuata juu ya wale waliokufuru, mpaka Siku ya Kiyama. Kisha marudieo yenu ni Kwangu, ndipo Nitawahukumuni katika yale mliyokuwa mkikhitalifiana.

NUKUU YA HADITHI

عن عبد الله بن عمرو قا ل قا ل رسول الله صلى الله عليه وسلم ينزل عيسى بن مريم إلى الأرض فيتزوج ويولد له ويمكث خمسا وأربعين سنة ثم يموت فيدفن معي في قبري فأقوم أنا وعيسى بن مريم في قبر واحد بين أبي بكر وعمر

Imesimuliwa na Hazrat Abdullah bin Amri r.a. ya kwamba Mtume saw alisema: atashuka Issa bin Maryam kwenye ardhi basi atoa na atajaliwa kizazi (cha kutumikia dini). Na atakaa ardhini miaka arobaini na mitano(yaani baada ya kutangaza madai ya kuwa ametumwa) kisha atafariki na atazikwa pamoja nami katika kaburi langu. Hivyo mimi na Issa bin Maryam tutainuka kutoka kaburi moja baina ya Abu Bakr na Umar. (Mishkat Bab nuzule Issa).

ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA[as]

Mwana Aliyeahidiwa

Seyyedna Ahmad a.s. anasema:(tafsiri ya kiarabu): Mtume saw alitoa bishara kwamba: kwa Yakini, Masihi Aliyeahidiwa ataoa na kujaliwa na kizazi. Kwa kweli imedokezwa ndani ya (maneno) hayo kwamba, kwa Yakini Allah mtukufu Atamjalia Mtoto mwema ambaye atakuwa mfano wa baba yake wala hatakuwa dhidi yake kisha atakuwa miongoni mwa watu watukufu wa Mwenyezi Mungu. (Aainae Kamalate Islam,Rohani Khazain J.5.UK.578)

Kisha anasema katika kitabu chake "Tuhfae Baghdad":(tafsiri): kuna dokezo kwenye (bishara) hiyo kuwa: huyu (Masihi Aliyeahidiwa) atazaliwa mwana mwema ambaye atakuwa mithili yake kutokana na sifa na ubora wake. (Tuhfae Baghdad,Rohani Khazain j.7.uk.209)

Hakika kwa ajili ya Mahdi wetu kuna ishara mbili ambazo hazijatokea (kwa kuhakikisha ukweli wa mdai ye yote) tangu ziumbwe mbingu na ardhi, nazo ni hizi: Mwezi utapatwa siku ya kwanza (miongoni mwa tarehe za kupatwa kwake) katika Ramadhan, na Jua litapatwa siku ya katikati (baina ya tarehe za kupatwa kwake) katika mwezi huo huo (wa Ramadhan). Wala hazijatokea ishara hizo (kwa ajili ya mdai ye yote) tangu kuumbwa kwa mbingu na ardhi. [Dar Kutni] (Sunan Dar Kutni, bab sifatu Salatil khusufi wal kusufi,j.1.uk.188)

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Ahmad Abdul Nasibu.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe: 1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

بسم الله الرحمٰن الرحيم

MUHTSARI WA HOTUBA YA IJUMAA ILIYOTOLEWA NA HADHRAT AMIR UL MOMENIN, KHALIFAT UL MASIH V ATBA - (KATIKA MASJID MUBARAK, ISLAMABAD (UK), TAREHE 04/02/2022

Kutoka uk. 1

Baada ya Tashahhud, Ta'awwudh na Surat Faatihah, Hadhrat Khalifatul Masih V, Hadhrat Amir ul Momeniin, Mirza Masroor Ahmad atba ('Ayyadahullahu Ta'ala Bi-Nasrihil Aziiz'); alisema kuwa, ataendelea kuangazia matukio kutoka katika maisha ya Hadhrat Abu Bakr (r.a):

Vita vya Banu Quraizah

Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba Hadhrat Abu Bakr (ra) pia alishiriki katika Vita vya Banu Quraizah. Walipokuwa wakielekea eneo la Banu Quraizah, Hadhrat Abu Bakr (ra) na Hadhrat Umar (ra) walipendekeza kwa Mtukufu Mtume (saw) kwamba kama angevaa vazi alilopewa ambalo lilichukuliwa kuwa zuri kwa viwango vya kidunia, basi watu wangependelea zaidi kuelekea kuukubali Uislamu. Mtukufu Mtume (saw) alikubali pendekezo lao, akisema kwamba hatakataa jambo ambalo wote wawili walikubaliana juu yake.

Mtukufu Mtume (saw) alisema kwamba Mungu amewafananisha wawili hao na Malaika Jibril na Mikaili, na kutoka kwa Mitume kama Nuhu (as) na Ibrahimu (as). Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba wakati huu, Waislamu wote walilazimika kula tende tu ambazo zilitumwa kwa ajili yao. Ilionekana kwamba Mtukufu Mtume (saw), Hadhrat Abu Bakr (ra) na Hazrat Umar (ra) pia walikuwa wakila tende tu, na Mtukufu Mtume (saw) alisema kwamba tende ni kitu kizuri sana cha kuliwa.

Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba kutokana na ndoto ambayo alijiona akizunguka Al-Kaaba, Mtukufu Mtume (saw) alitoka pamoja na masahaba 1,400 kuelekea Ka'aba. Hata hivyo, Mtukufu Mtume (saw) alifahamu kwamba watu wa Makka walipanga kuwazuia Waislamu wasiingie. Mtukufu Mtume (saw) aliposhauriana na masahaba, Hadhrat Abu Bakr (ra) alisema kwamba waendelee kwani nia yao haikuwa kupigana, na kama mtu yeyote angejaribu kuwazuia, basi watajilinda wenyewe.

Mkataba wa Hudaibiyah

Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba wakati wa Mkataba wa Hudaibiyah, Urwah alikwenda kwa Mtukufu Mtume (saw) ili kujadiliana juu ya masharti ya mkataba.

Alimwambia Mtukufu Mtume (saw) kwamba kama Maquraishi wangekuwa washindi, basi masahaba wangemwacha Mtukufu Mtume (saw).

Kusikia hivyo, Hadhrat Abu Bakr (ra) hakuweza kuvumilia na akamwambia Urwah kwamba aondoke na arudi kwenye masanamu yake, akimaanisha kwamba wakati waabudu masanamu walikuwa wamejitolea kwa masanamu yao ya uwongo, vipi Waislamu ambao walikuwa wamekita mizizi katika ukweli na kumwamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake (saw) wangemtelekeza? Urwah alisema kwamba hatajibu jambo hili, kwani Hadhrat Abu Bakr (ra) alikuwa amemfanyia fadhila juu yake hapo kabla ambayo alikuwa bado hajailipa.

Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba juu ya masharti ya Mkataba wa Hudaibiyah, Hadhrat Umar (ra) alimuuliza Mtukufu Mtume (saw) kwamba kama yeye alikuwa mkweli, basi kwa nini Waislamu walikuwa wanakubali masharti hayo wakati Mtukufu Mtume (saw) alisema kwamba Waislamu watakwenda kwenye Kaaba? Mtukufu Mtume (saw) alisema kwamba kwa kutegemea ndoto yake, hakuwa amesema kwamba kwa hakika watafika Ka'aba mwaka huo huo, na akasema kwamba hakika yeye atafuata mapenzi ya Mungu.

Baadaye, wakati Hadhrat Umar (ra) alipotamka vivyo hivyo kwa Hadhrat Abu Bakr (ra), yeye pia alitoa jibu sawa na Mtukufu Mtume (saw) na akasema kwamba kamwe hatakwenda kinyume na matakwa ya Mwenyezi Mungu. Baadaye, Hadhrat Umar (ra) alisema kwamba alijutia kuuliza maswali kama hayo na akafunga ahadi juu yake mwenyewe kufanya matendo mema daima kama kafara ya kauli yake hiyo.

Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba kulikuwa na nakala mbili zilizoandikwa za Mkataba wa Hudaibiyah; moja kwa kila upande.

Pia walikuwepo mashahidi ambao walitia saini mkataba huo, miongoni mwao ni Hadhrat Abu Bakr (ra).

Hadhrat Abu Bakr(ra) Aongoza Msafara wa kuelekea Banu Fuzara

Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba Hadhrat Abu Bakr (ra) alishiriki katika Msafara wa Banu Fuzara, ambao walikuwa wakipanga njama dhidi ya Waislamu. Kwa mujibu wa baadhi ya riwaya, Mtukufu Mtume (saw) alimteua Hadhrat Abu Bakr (ra) kama kiongozi wa msafara huu. Vita na makafiri vikatokea ambapo Waislamu walipata ushindi.

Kushiriki katika Vita vya Khaibar

Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba Hadhrat Abu Bakr (ra) pia alishiriki katika Vita vya Khaibar. Waislamu walizingira ngome zao kwa zaidi ya mausiku kumi na hatimaye wakafanikiwa kuzishika. Wakati huu, Mtukufu Mtume (saw) alikuwa akiugua maumivu ya kipandauso na hakutoka nje kwa siku kadhaa. Mtukufu Mtume (saw) alimtuma Hadhrat Abu Bakr (ra) kuelekea kwenye moja ya ngome ambako vita vikali vilianza, lakini jeshi la Waislamu lilishinda chini ya uongozi wa Hadhrat Abu Bakr (ra).

Hadhrat Abu Bakr(ra) Aongoza Msafara kwenda kwa Banu Kilaab

Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba Hadhrat Abu Bakr (ra) pia alishiriki katika Msafara wa Najd, ambapo Banu Kilaab walisimama dhidi ya Waislamu. Mtukufu Mtume (saw) alimteua Hadhrat Abu Bakr (ra) kama kiongozi wa msafara huu pia.

Kutekwa kwa Makka

Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba Hadhrat Abu Bakr (ra) pia alishiriki katika Utekaji wa mji wa Makka. Moja ya makabila washirika wa Maquraish walikuwa wametenda kinyume na Mkataba wa Hudaibiyah.

Baada ya hayo, siku moja Hadhrat Abu Bakr (ra) alikwenda kumuona binti yake Hazrat Aisha (ra) na akamwona akitayarisha vitu vya Mtukufu Mtume (saw).

Wakati huo, Hadhrat Aisha (ra) hakujua ni wapi Mtukufu Mtume (saw) alikusudia kwenda. Wakati huo huo, Mtukufu Mtume (saw) alifika, na akamjulisha Hadhrat Abu Bakr (ra) kuhusu nia yake ya kwenda Makka, lakini akamuagiza kutolifichua jambo hili kwa mtu yeyote.

Baadaye, Mtukufu Mtume (saw) aliwatangazia Waislamu kwamba wajiandae kwa ajili ya safari, lakini bado hakuwaeleza ni wapi wangeenda. Mtukufu Mtume (saw) pia alihakikisha kwamba hakuna mtu yeyote kutoka kwa Maquraishi anayejua kuhusu maandalizi ya Waislamu.

Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba Waislamu walipofika sehemu iitwayo Marruz-Zuhrah ambayo ni kilomita 25 kutoka Makka, Mtukufu Mtume (saw) aliwaagiza Waislamu kuwasha mioto elfu kumi. Maquraishi wakaingiwa na wasiwasi, kwani walikuwa na hakika kwamba vita vitatokea.

Abu Sufyan aliwaendea Waislamu ili kujua nini kinatokea, na kutafuta usalama. Baada ya kuwasili, Abu Sufyan na wajumbe wengine wawili pamoja naye walipelekwa kwa Mtukufu Mtume (saw) na wakasilimu.

Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba ataendelea kusimulia matukio haya katika khutba zijazo. Inshallah.

AHMADIYYA YATIMIZA MIAKA 133 (1889 - 2022)

Kutoka uk. 1

Hazrat Mirza Tuhir Ahmad rha na sasa tunaye Khalifatul Masih wa tano (ATBA)

Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya ndiyo jumuiya ya Kiislam inayoongoza kukataa kabisa ugaidi. Zaidi ya karne moja iliyopita, Mirza Ghulam Ahmad alitangaza kwa msisitizo kwamba "jihadi kwa upanga" haina nafasi katika Uislamu. Badala yake aliwafundisha Waislamu kufuata Qur'ani na mfano wa Mtume Muhammad (saww) na kuutetea Uislamu kwa "jihadi ya kalamu" isiyo na damu, yenye kutumia maarifa. Kwa hiyo, Mirza Ghulam Ahmad aliandika zaidi ya vitabu 80 na makumi ya maelfu ya barua, akatoa mamia ya mihadhara, na kushiriki katika mijadala mingi ya hadhara. Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya inaendelea kutumia elimu kuwarekebisha Waislamu kwa amani na kuhuisha Uislamu duniani kote.

Mirza Ghulam Ahmad aliwakumbusha Waislamu juu ya ahadi ya Mwenyezi Mungu ya kuulinda Uislamu kupitia ukhalifa (taasisi ya kiroho ya urithi wa utume).

Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya inaamini kwamba ukhalifa wa Kiislamu pekee ndio unaweza kuwaunganisha wanadamu kwa amani. Makhalifa watano wamemrithi Mirza Ghulam Ahmad tangu kufariki kwake.
Khalifa wa sasa, Mirza Masroor Ahmad, anaishi Uingereza na anahudumu kama kiongozi mkuu wa kiroho na utawala wa jumuiya. Chini ya uongozi wa ukhalifa, Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya imejenga zaidi ya misikiti 16,000, shule 600 na hospitali 30. Imetafsiri Kurani Tukufu katika lugha zaidi ya 70. Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya inaeneza mafundisho ya kweli ya Uislamu ya amani na uvumilivu kupitia chaneli ya televisheni ya saa 24 ya satelaiti (MTA), Mtandao (www.alislam.org), na magazeti (Islam International Publications). Ipo mstari wa mbele katika kutoa misaada ya majanga duniani kote kupitia Humanity First, Taasisi ya kujitolea bila kuhitaji faida.

Wako,
Raghib Zia-ul Haq,
Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya Tanzania

BISMILLAHI RAHMAAN RAHIIM
JAMIA AHMADIYYA WAADHIMISHA SIKU YA MWANA ALIYEAHIDIWA R.A

Kutoka uk. 12

Shairi hilo lilikuwa na ujumbe usemao,"Twamuombea mema khalifa wetu wa pili".
Baada ya shairi hili ilifuata hotuba yenye madhumuni isemayo," Kuthibitisha jinsi mwana aliyeahidiwa r.a alivyojazwa elimu ya ndani na ya nje". Hotuba hiyo ilitolewa na Maulana Sheikh Ayaaz.A.Dogar sahib.Sheikh sahib kwa ustadi mkubwa aliwasilisha hotuba yake ambayo kwa hakika iliwasisimua sana wasikilizaji. Sheikh sahib alianza kwa kueleza hali ya afya ya Hadhrat Musluh Mau'ud r.a katika utoto wake jinsi alivyokuwa anaumwaumwa na maendeleo yake jinsi yasiyoridhisha katika masomo yake ya shule, lakini matokeo ya baadae yalidhibitisha pasina shaka yoyote kuwa kweli mwana huyu alijazwa na Allah elimu ya ndani na ya nje.
Sheikh sahib alijaribu kuorodhesha vitabu vya fani mbalimbali kama nvile sayansi, uchumi, kilimo n.k alivyopata kusoma Hadhrat Muslih Mau'ud r.a na akasema kwa ujumla ya vitabu alivyosoma ni Zaidi ya 7521 na hivi ni vile tu vilivyorekodiwa.
Lakini yeye mwenyewe [Hadhrat Muslih Mau'ud r.a] akizungumza katika mkutanao na wanafunzi wa jamia,alisema kuwa kwa usiku mmoja anasoma Zaidi ya kurasa mia nne za kitabu,na hadi wakati huo amesoma jumla ya vitabu 20000.Na akasema kuwa hakuna mtaalamu yeyote wa dunia anaweza kuleta hoja yoyote katika fani yoyote isipokuwa atamjibu kikamilifu na kumaliza kabisa ubishi wake.
Baada ya hotuba hiyo,kiongozi wa hafla Principal sahib alisimama na kutoa nasaha chache kwa wanafunzi na wasikilizaji wote kwa ujumla .Katika nasaha zake Principal sahib alisema kuwa pamoja na kwamba Allah alimsaidia huyu mwana, lakini bado tunaona jisi mwana aliyeahidiwa r.a alivyofanya bidii katika kusoma.Na alikuwa akitoa hotuba masaa sita had inane bila ya kuchoka na wasikilizaji nao walikaa kwa utulivu kumsikiliza bila hata kutoka kikaoni.Na kwa nukta hiyo,aliwaasa wanafunzi na wasikilizaji wote kutilia maanani suala la kujisomea tena kwa bidii. Mwisho mheshimiwa mkuu wa chuo aliongoza maombi na kufunga kikao.Kisha washiriki walisali sala za adhuhuri na alasir kwa pamoja.

MAHUBIRI KATIKA MJI WA BAGAMOYO

wa fadhila na Rehema za Allah, Tarehe 13 Febuari, 2022, Majlis Ansarullah kwa kushirikiana na Majlis Khuddamul Ahmadiyya, walifanya ziara katika Mji wa Bagamoyo Mkoa wa Pwani.

Mji wa Bagamoyo
Bagamoyo ni katika miji ya kale hapa nchini na ni mji wenye vivutio vingi vya utalii. Mji huu ulikuwa ni maarufu hapo kale kutokana na kuwa kitovu cha biashara ya watumwa katika pwani ya Afrika ya Mashariki na hivyo ulifikiwa na wageni wengi hususani Waarabu. Hivyo mji huu wa Bagamoyo ni katika miji iliyopokea Uislam tokea siku za mwanzo za Islam.

Katika ziara hiyo iliandaliwa mipango ya aina mbili kwa ajili ya utekelezaji;
(1) Mahubiri
(2) Picnic

1. Katika Mahubiri,
Wana Ansarullah, Khuddamul Ahmadiyya na Atfalul Ahmadiyya,wakitumia baskeli 26 za kukodi na wengine wakitembea kwa miguu, waligawa vipeperushi katika vitongoji vya mji huo kwa muda wa saa moja na nusu. Alhamdulillah.

Mahubiri yalifanyika kwa mafanikio sana huku wakifuatilia kuona iwapo kuna athari ya mahubiri ya mara ya kwanza yaliyofanyika katika mji huo miezi mitatu iliyopita.



Hakika hapakuwa na upinzani zaidi ya hoja za hapa na pale ambazo zilipatiwa majibu stahiki. Jumla ya vipeperushi 4200 vilitawanywa kwa muda huo. Maswali yaliyoulizwa yalipatiwa majibu stahiki.
Jumla ya washiriki walikuwa 77 ikiwa ni Ansarullah 24, Khuddam 34 na Atfal 17.
KAkiwaaga kwa ajili ya safari, Amir Sahib Sheikh Tahir Mahmood Choudhry, aliwaongoza kwa maombi na Aliwatakia safari njema na kuwaombea heri na baraka katika mahubiri hayo.
Safari ilianzia Makao makuu ya Jamaat Masijid Salaam mnazi mmoja Dar es Salaam majira ya saa mbili asubuhi na kuwasili bagamoyo Majira ya saa tano.

Sadr Ansarullah Bw. Ally Hamisi Mbambwa akiwakumbusha wajibu wao katika safari hiyo, aliwaasa wabaki kwenye nidham ya jamaat kwa kuhubiri kwa upendo na amani na kila mmoja afungamane na kundi alikopangiwa bila kuzurura ovyo. Aliwaagiza kuwaangalia Atfal na kuwaongoza kuwaongoza katika Mahubiri hayo.

Baada ya kufanya mahubiri na kuhakikisha watu wote wamerudi salama, Majira ya saa nane mchana, waliekea katika fukwe ya bahari kwa ajili ya picnic.

2. Picnic
Tulifika ufukweni mwa bahari katika beach nzuri ya Bagamoyo na jambo la kwanza ilisaliwa sala ya Adhuhuri na Alasiri iliyoongozwa na Mwl Ally Rashid sahib.
Baada ya sala watu walivaa mavazi ya michezo na kuanza michezo mbalimbali ikiwemo kuogelea, Beach soccer na riadha za ufukweni za mbio fupi.
ulifika wakati wa ziafat. Wakati ambao uliongeza furaha na ladha ya shughuli nzima. kuku wa kuchoma, Ndizi mzuzu, chips, soda na maji ni baadhi ya vyakula vilivyoandaliwa. Kila mmoja alipewa kifurushi chake. Hakika Ilikuwa ni package ya nguvu na ya maana kama vifurushi vya Tigo au TTCl vilivyo sheheni kila kitu ikiwemo pilipili, kachumbari na chachadu ili kuongeza ladha.
Baada ya dhiafati (chakula) watu walirudi kwenye maji na michezo mingine iliendelea.
Hatimaye tulikusanyika kwa pamoja ambapo Sadr Khuddam Bw. Rahim Iddi Mwanga alitoa neno la shukrani kwa kuwashukuru watu wote waliohudhuria kwa kushiriki mahubiri haya na picnik.

Inaendelea uk. 8

Inatoka uk 1

IMANI NA UTUMIAJI WA AKILI



Hussein Mukwahe

Kwa kawaida mwanadamu hupata habari kupitia vyanzo vikuu viwili kuona au kisikia na Akili hufanya upembuzi yakinifu ili kupata uhakika wa jambo husika, na Jambo hilo likikosekana uhakika akili hulikataa na mwanadamu hawezi kulikubali.

Na mungu ndivyo anavyotaka mtu atumie kipawa alicho pewa (AKILI) kutafakari mambo na usipofanya hivyo anasikitika sana.

Watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa; kwa kuwa wewe umeyakataa maarifa, mimi nami nitakukataa wewe, usiwe kuhani kwangu mimi; kwa kuwa umeisahau sheria ya Mungu wako, mimi nami nitawasahau watoto wako. Hoseo 4:6;
Je ham itafakari Qurani hii? 4:83;

Tunaposhika misingi ya imani tuhakikishe tunapoulizwa maswali na waumini utolewe ushahidi wa maandiko na maelezo yanayoingia Akilini na kinyume na hapo utaleta mshangao na utata kwa waumini na watu wengine,

Wewe ni mtu wa mungu lakini vitu vya mungu huvijuwi na huvielewi katika utendaji wake. Hicho ni CHANZO CHA MWANADAMU CHA KUKATAA UWEPO WA MUNGU,

Kwa mfano Mwaka 1564 -- 1642; mwanasayansi. Galileo (mkatoliki) ni kanisa mama alipoeneza uvumbuzi wake kuhusu mfumo wa jua, dunia, na sayari, ya kwamba ni sayari zinazozunguka, ikalikasirisha Kanisa kwa uvumbuzi wake huo ulipinzana na utambuzi wa kanisa kuhusu utaratibu wa jamii ya jua, ardhi, na sayari nyingine,

Alitishwa vikali na kulazimishwa kukanusha uvumbuzi wake wa kisayansi. La sivyo angeweza kuuawa kwa kuteswa vibaya,
Hata hivyo alihukumiwa kifungo cha maisha mpaka mwisho wa maisha yake.

Na baada ya kupita karne tatu na nusu ikaondolewa hukumu hiyo mwaka 1992, Baada ya mjadala wa miaka 12, ktk kamati iliyondwa na papaJohn poul ll, Hayo ni mapungufu makubwa ya uwelewa

MISINGI YA IMANI YA UKRISTO NI HII HAPA

(1) Adamu ni mtu wa kwanza na binadamu wote tumetokana na yeye
(2) Watu wote tuna dhambi ya kurithi kutoka kwa Adamu.
(3) mungu kamtoa mwanawe mpendwa kuukomboa ulimwengu.
n.k, Adamu kuwa mtu wa kwanza na binadamu wote tumetokana na yeye Maandiko ya vitabu vya Dini vinakataa, pia Akili inakataa

Tukitalii biblia inasema
Hiki ndicho kitabu cha vizazi vya Adamu. Siku ile Mungu alipoumba mtu, kwa sura ya Mungu alimfanya; mwanamume na mwanamke aliwaumba, akawabariki akawaita jina lao Adamu, siku ile walipoumbwa.
Mwz 5:1 -- 2;
Kwa maana hiyo kila tabaka la udongo walikuwa na Adam wao,

wana wa Mungu waliwaona hao binti za wanadamu ya kuwa ni wazuri; wakajitwalia wake wo wote waliowachagua.
Nao Wanefili walikuwako duniani siku zile;tena ,baada ya hayo ,wana wa Mungu walipoingia kwa binti za binadamu,wakazaa nao wana;hao ndiyo waliokuwa watu hodari zamani ,watu wenye sifa. Mwz 6:2, 4; hao Wana wa mungu walikuwa na adamu wao,

Na Qur'an Tukufu inatilia nguvu jambo hili kwa kusema
Na Mwenyezi Mungu Akawaotesheni katika ardhi kama mimea: Kisha Atawarudisheni humo na Atawatoeni tena kwa njia maalum. 71:18 -- 19;
Kama ni mnazi ulianza mnazi, vivyo hivyo, mparachichi, mwembe, mkorosho, nk,

Kudhani mmea mmoja ndio chanzo cha mimea yote hiyo kiakili haikubaliki, pia kwa mwanadamu haingii Akilini. Mwaafrika, mchina,mwingereza, muhindi.nk.
Tumetokana na mtu mmoja ADAMU.

Vitabu vya Dini vinakataa pia na Akili haikubali.

Kwa uthibitisho kukataa kwa AKILI wanandoa ni waafrica mwanamke anajifungua mtoto wa kichina Je ukawa wewe, pakoje hapo !!??; Hata DNA ziko tofauti, kwa nini hazifanani !!??.

WATU WOTE TUNADHAMBI YA KULISI KUTOKA KWA ADAMU

Msingi huu umetoka kwa adamu baada ya kufanya kosa na ndio maana wanalazimisha watu wote tumetokana na yeye ili kutulithisha zambi yake, na tunakufa kwa sababu ya dhambi hiyo.

Lakini maandiko yanakataa pia na Akili,
Mababa wasiuawe kwa ajili ya watoto wao, wala watoto wasiuawe kwa ajili ya baba zao; kila mtu na auawe kwa ajili ya dhambi yake mwenyewe. Kumb 24:16;
Kwa sababu dhambi ni kitendo cha mtu binafsi,

Na kuna uwezekano Baba akawa mtenda dhambi, mtoto akawa mtenda haki, aau ikawa kinyume chake, kama yanavyothibitisha maandiko,

Roho itendayo dhambi, ndiyo itakayokufa; mwana hatauchukua uovu wa baba yake, wala baba hatauchukua uovu wa mwanawe, haki yake mwenye haki itakuwa juu yake, na uovu wake mwenye uovu utakuwa juu yake. Ezekieli 18:20;
Na ukianzia 18:4 -- 30; imefafanua vizuri sana. Na Qur'an Tukufu imesema m bebaji hatabeba mzigo wa mwingine 17:16;.
Ki Akili haiwezekani kosa lifanywe na mtu mwingine ahukumiwe mtu mwingine,huo sio uadilifu.
Mwanadamu tu hawezi kufanya kioja hiki sembuse mungu.

MUNGU KUMTOA MWANAWE WA PEKEE KUUKOMBOA ULIMWENGU

Maana ya kukombolewa ni mtu kuondokana na adhabu, mateso, baada ya kuhukumiwa kwa makosa aliyoyafanya au kwa sababu nyingine yoyote ile iwaya, Inapo tolewa vidia kwa jambo husika mtu huyo adhabu
Na mateso hayapatikani Tena kwa mtu huyo.
MUNGU katoa adhabu kwa watu wote baada ya Adamu na Hawa kufanya dhambi, Mwanamume kupata ridhiki yake kwa kutoka jasho na mwanamke kuzaa kwa uchungu.

MUNGU huyo huyo akawahurumia watu wake kwa adhabu aliyowapa akamtoa mwanawe anaempenda wapekee ili kuukomboa ulimwengu.
Sasa ili uhusike na Ukombozi huo unatakiwa kumkubali na kumwamini, adhabu na mateso hayapatikani tena kwako.
Je kuna mkristo yupi awe Mwanamume au mwanamke, aliye mwamini mtoto huyo aliyeondokana na adhabu hizo !!!???

Kwa bahati mbaya zaidi na mtoto mwenyewe akawa mjinga kupitiriza anasema anajiua ili watu wakombolewe na hapo hapo anageuka anasema, Lakini nendeni, mkajifunze maana yake maneno haya, Nataka rehema, wala si sadaka; kwa maana sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi. Mt 9:13;

Tutumie Akili ya kawaida tu wewe umempeleka mgonjwa hospital yuko mahututi na daktari kwa kumhurumia mgonjwa anatangaza kujiua ili mgonjwa apone, je daktari huyo utamwonaje. !!!???

Ukikusanya taarifaha hizi, Watu wote tumetokana na Adamu, watu wote tuna dhambi ya kurithi, mungu kamtoa mwanawe wa pekee kuukomboa ulimwengu, Tukio la mwanawe na Tukio la bwana Galileo ni ushahidi tosha kwa mtu mwenye Akili timamu na uwezo wa kufikiri kutambua, MISINGI YA IMANI YA UKRISTO NI CHANZO CHA MWANADAMU CHA KUKATAA UWEPO WA MUNGU.

Iwe mkristo achana na misingi ya imani inayokuwa chanzo cha kukataa kwa Uwepo wa mungu
Uungane na mkuu wa ulimwengu ambae ameshahukumiwa ili umjue mungu Wa pekee aliye mtuma YESU KRISTO. Yoh 16:11, na You 17:3;
Na neno langu la mwisho ni UPENDO KWA WOTE BILA YA CHUKI KWA YEYOTE.

Bwana Hussein ameanzisha majadala ambao unatutaka nasi tutoe maoni yetu ili kurutubisha fikra. Kutofautiana katika fikra ni jambo la neema kubwa hata bustani inakuwa na maua yenye rangi nyingi na kwa kufanya hivyo madhari ya bustani hiyoinafutia.

Inachosha na haifutii bistani yenye maua yaliyo narangi moja utamaduni wa kubadilishana mawazo kutofautiana bila kukwaluzana lakini kuheshimu fikra za mwingine na kutoa hoja ilio bora zaidi ndio njia ya kuleta maendeleo katika jamii. Tunakaribisha uwanja u wazi kwa aliye na mchango wa mawazo.

Muhariri

Bustani ya Washairi



(Sh. Shahab Ahmad, Dar es Salaam)

KASIDA
ya kumsifu Mtume Mtukufu (saw)

(sehemu ya 1)

(makala hii imechapishwa katika toleo hili sawa na umuhimu wa siku ya Masihi Aliyeahidiwa a.s nayo itaendelea pia katika matoleo yajayo, Mhariri)

Seyyid Ahmad (as) wa Qadian ni Imamu wa zama ambaye alitabiriwa na Mtume wetu Mtukufu Hadhrat Muhammad (saw). Maandishi yake yamejaa mifano mingi ya kumsifu Bwana wetu Mtukufu (saw). Mbali na vitabu vyake, aliwahi kutunga mashairi mengi ya Kiarabu, Kiurdu na Kiajemi akizungumzia maudhui hayo. Miongoni mwa tungo hizi ni kasida maarufu ya Kiarabu inayojulikana kama Yaa aina faizillahi wal'irfani. Kasida hii ilitungwa mwaka 1893 na kuchapishwa katika kitabu cha Aina Kamalati Islam yaani Kioo cha Sifa za Uislamu.

Hii ni kasida ya kwanza iliyotungwa na Hadhrat Masihi aliyeahidiwa (as) katika lugha ya Kiarabu. Wanajumuiya wote watoto kwa wakubwa huwa wanajitahidi kukumbuka kwa moyo beti za kasidi hiyo kwa Kiarabu. Kasida hii husomwa sana katika hafla za Jumuiya duniani kote na inaonesha jinsi Seyyid Ahmad (as) alivyokuwa na hisia za hamu na upendo kwa ajili ya Fahari ya Manabii Mtume Mtukufu (saw). Raghba ya aina hii ndiyo aliyotaka kuizalisha ndani ya watu wa Jumuiya yake. Kwa hiyo, tukiimba au kusoma kasida hii adhimu yatupasa kuzifahamu maana zake ili umuhimu wake nao ueleweke vizuri.
Safari moja Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) alisema kuhusu kasida hii:

"Kasida hii imekubaliwa mbele ya Mwenyezi Mungu naye Aliniambia kuwa yeyote atakayehifadhi kasida hii na kuisoma kwa kudumu, mimi nitajaza vizuri upendo wangu na upendo wa Mtume Mtukufu (saw) moyoni mwake na nitamjaalia ukaribu wangu."

Pia aliongeza:

"Mtu yeyote atakayehifadhi kasida hii, kumbukumbu zake zitabarikiwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu."

Hapa chini msomaji anapewa nafasi ya kuzipitia beti moja moja za kasida hii ambayo imesheheni lulu zenye thamani za Kiarabu. Kila ubeti umeandikiwa tafsiri yake kwa lugha ya Kiswahili. Katika tafsiri hii imezingatiwa kuhawilisha maneno yote ya Kiarabu huku lengo likiwa ni kufikisha ujumbe uliomo katika kila utungo. Aidha, kila ubeti umewekewa ufafanuzi na maelezo kwa ufupi.

1

يَا عَيْنَ فَيْضِ اللهِ وَ الْعِرْفَانِ
يَسْعٰى إِلَيْكَ الْخَلْقُ كَالظَّمْآنِ

Tafsiri: *Ewe uliye chemchemi ya neema na maarifa ya Allah, mahuluku hukimbilia kwako kama mtu aliyeshikwa na kiu.*

Maelezo: *Katika ubeti huu, Mtume Mtukufu (saw) alielezwa kisitiari kuwa chemchemi na chanzo cha kupata neema na fadhila za Allah kwa sababu yeye ni mbora wa Manabii wote. Baada ya ujio wake upokeaji wa neema za Allah unategemea kumfuata yeye (saw). Kimsingi, alifuata kikamilifu mafundisho ya Allah katika maisha yake yote naye ndiye alitufundisha namna za kuelewa maarifa ya Allah. Chemchemi hii ya kiroho iko wazi kwa ajili ya watu wote. Ndiyo maana, wale wanaoshikwa na kiu ya kiroho na kutafuta suluhisho lake hujitahidi kufuata njia yake na kuiga mfano wake uliotukuka.*

2

يَا بَحْرَ فَضْلِ الْمُنْعِمِ الْمَنَّانِ
تَهْوٰى إِلَيْكَ الزُّمَرُ يَا نَيْرَانِ

Tafsiri: *Ewe uliye bahari ya fadhila za Mungu Atoaye neema na Manani, makundi ya watu huja mbio kwako wakibeba ndoo.*

Maelezo: Katika mshororo wa kwanza sifa mbili za Allah (swt) zimetajwa ambazo ni Mun'im na Mannan. Mun'im ni jina linalomaanisha, mtoaji wa neema na sifa ya Mannan inatokana na kitenzi manna (مَنَّ) ambayo maana yake ni Mpaji Mkuu. Mtume Mtukufu (saw) alibainishwa kuwa bahari iliyojaa fadhila za sifa hizi mbili za Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo watu wanaotaka kuchota maji ya kiroho kutoka bahari hiyo humwelekea yeye wakikusanyika kama makundi ikiwa wamebeba ndoo zao. Neno زُمَر *lamaanisha kundi la watu ambalo wingi wake ni* زُمَرٌ.

3

يَا شَمْسَ مُلْكِ الْحُسْنِ وَالْإِحْسَانِ
نَوَّرْتَ وَجْهَ الْبَرِّ وَ الْعُمْرَانِ

Tafsiri: *Ewe uliye jua la ufalme wa uzuri na hisani! Umenawirisha pande zote za pori na mastakimu.*

Maelezo: *Hapa Mtume Mtukufu (saw) ameelezwa kuwa mtu aliyezidi katika uzuri na ukarimu wake kuliko watu wote. Tukisoma kuhusu maisha yake anajitokeza kuwa mwenye shani ya kipekee katika sifa hizi mbili. Vilevile, katika ubeti huu yeye alimithilishwa na jua. Yaani jinsi jua linavyoangaza dunia nzima vivyo ndivyo mafundisho ya Mtume Mtukufu (saw) yamewalenga watu wote duniani bila ubaguzi wowote. Katika mshororo wa pili wa ubeti huu, sifa yake nyingine imebainishwa kuwa baada ya kupata nuru kutoka kwa Mwenyezi Mungu, hakuwanyima wengine bali akaeneza nuru yake duniani kote. Wanadamu si pekee bali viumbe vyote vilinufaika na nuru yake.*

4

قَوْمٌ رَاَوْكَ وَ اُمَّةٌ قَدْ اُخْبِرَتْ
مِنْ ذٰلِكَ الْبَدْرِ الَّذِيْ اَضْبَانِيْ

Tafsiri: *Kaumu (ya watu) ilikuona na umati mmoja (wa watu) ulipewa taarifa ya ile badiri iliyoniraghibu sana.*

Maelezo: *Katika ubeti huu, Mtume Mtukufu (saw) alipewa sifa ya Badiri yaani mwezi mpevu unaong'aa sana kutokana na nuru yake. Masahaba waliomwona huyo bwana mwenye sifa kemkemu, walikaa pamoja naye na wenyewe wakashuhudia ukweli wa mafundisho matukufu aliyoyaleta. Baada ya kufariki kwake nuru hii iliendelea kusambaa duniani na wote wasiojaaliwa kumwona katika uhai wake wakapata kupokea nuru ya mafundisho yake.*

Mshairi anaeleza hali yake mwenyewe kwamba jinsi ambavyo kwa kusoma kuhusu maisha ya Mtume huyo (saw) amevutiwa na nuru yake. Neno linaloonesha upendo wa hali ya juu ni أَبْصٰنِيْ *kwamba Mtume (saw) amenifanya kuwa na raghba naye ambayo ilipita kiasi.*

5

يَتَكَوَّنُ مِنْ ذِكْرِ الْجَمَالِ صَبَابَةٌ
وَ تَأَلُّمًا مِنْ لَوْعَةِ الْهِجْرَانِ

Tafsiri: *Wao kutokana na hamu kubwa hulia wakikumbuka uzuri (wako) na (vilevile) kwa kujisikia uchungu utokanao na huzuni ya utengano.*

Maelezo: *Kama ilivyoelezwa katika ubeti uliopita kwamba baadhi ya watu waliishi pamoja na Mtume Mtukufu (saw) na kuna wengine waliopata taarifa yake katika zama za baadaye. Wote wanampenda na kumkumbuka sana kutokana na upendo walio nao kwa ajili yake. Pamoja na kuwa na sura na haiba ya kupendeza, Mtume Mtukufu (saw) alikuwa mwenye mienendo mizuri na khulka njema kabisa. Kwa hiyo, watu wanalia wakikumbuka uzuri wake wa nje na wa ndani. Vilevile, watu husikitika na kulia sana kwa sababu hawawezi tena kuungana naye kimwili.*

ISIPOKUWA ALLAH[sw]

Ile hali ya kudumu, kuwepo pasipo kwisha
Jambo hili ni la haramu, katika yetu Maisha
Linalodumu dawamu, kwa kiapo ninabisha
Yalivyokwisha mengine, nalo hili litakwisha.

Hata hili litakwisha, yalivyokwisha mengine
Mazito yaliyokwisha, membamba nayo manene
Rabi ametuepusha, twabaki kula senene
Mwisho wa dhiki faraja, ahadi tuliyopewa.

Mahmood Hamsin Mubiru – Wamamba
Kiwalani – Dar es salaam.

DUA_MWANANA

Ya Rabi nifunze Kina, sifa nisizizoee
Nipe nguvu za Ujana, Na akili za Mzee
Na hekima za Ujana, Uwezo wa Kipekee
Kwa marefu na mapana, Maovu niyakemee
Kwa Kazi zenye mwanana, Na malengo nifikie

Shabani A. Shunda
Shunda Mshundia Wana - Daluni Tanga

SHANGWE

Shangwe na vigelegele, uweza kukuadaa ukamba u mteule wote wakusangilia siza wa enzi za kale mfano katuachia hata nawe burutusi Ai! dunia dania.
Msebeni bi Shabaani Bushumba

SEYIDNA ABUBAKAR (RA)

MAISHARA YA HAZRAT ABUBAKAR SADIQra

Huu ni fululizo wa vitabu vilivyo andikwa na kwa ajili ya Watoto ili wafahamu watu mashuuri katika dini ya Islamu. Ifuatayo ni tafsiri ya *Hadhrat Abubakar Siddiq* Kimefasiriwa kutoka Kiurudu kuja kiingereza na Mirza Ghulam Ahmad na Syed Mubashati Ahmad Ayaz. Na sasa kimefasiriwa katika kiswahili. Ni matumaini yetu ya kwamba vijana wetu watapatavitabu vya maana vya kusoma.
Malalamiko waliyonao vijana wetu nikukosa vitabu vizuri na vyenye maadili kwa ajiuliya kuimareisha katika imani na masomo yao matarajio yetu makubwa ni kwamba wazazi wataimiza vijana wasome vitabu hivi na litakuwa jambo jema wakituletea maoni ili kwa pamoja tuweza kuwasaidia vijana wetu wajenge utamaduni wa kupenda kusoma utamaduni amabo unaonyesha kupotea siku hadi siku. Karibuni kwenye ukurasa wenu

1

KUJITOLEA KWA HALI YA JUU

Kuna kipindi Mfalme wa Rumi -Heraclius aliwashawishi Waarabu na Wasyria wasiokuwa Waislam kuwashambulia Waislam na akaahidi kuwapa msaada. Habari hizi zilipomfikia Mtukufu Mtume Muhammad (saw) akaamua kwamba badala kusubiri washambuliwe, wao watakuwa wakwanza kushambulia. Hivyo mtukufu Mtume (saw) akaanza matayarisho ya vita. Ikumbukwe kwamba wakati huo serikali ya Kiislam haikuwa na vyanzo vya kupata pesa. Hivyo ilipojitokeza haja Mtukufu Mtume (saw) aliwaomba Waislam wajitolee kwa ajili ya Allah kwa fedha au kwa njia yoyote nyingine. Katika tukio hili Mtukufu Mtume Muhammad (saw) aliwataka Masahaba watoe michango yao.



Masahaba wote wa Mtukufu Mtume Muhammad (saw) waliitika mwito huo na kutoa kila mmoja sawa na uwezo wake. Baadhi walitoa dinari 1,000 wengine walitoa 4,000 baadhi walitoa nusu ya mali yao, hata hivyo palikuwa na sahaba ambaye alikusanya kila kitu kilichokuwepo nyumbani kwake na akakileta kwa Mtukufu Mtume (saw) kwa ajili ya harakati hizo. Baada ya kuona vitu vyote alivyoleta Mtukufu Mtume (saw) alimuuliza je umeacha chochote nyumbani kwa ajili ya mkeo na watoto? Kwa swali hilo alijibu; “nimewaachia wao Allah na Mtume wake (saw)”.
Je unamfahamu sahaba huyo mtukufu? Jina la sahaba huyo ni Abubakar (ra). Alikuwa miongoni mwa watu wa mwanzoni kumkubali Mtukufu Mtume Muhammad (saw) na pia alikuja kuwa Khalifa wake wa kwanza. Na kwa hakika katika dini ya Islam jina linalojulikana sana ni la Seyidna Abubakar (ra). Sio tu kwamba anaheshimika katika historia ya Islam la hasha! Yeye pia anaheshimika katika historia ya dunia kwani ni miongoni mwa watu waliobadili mkondo wa historia.

2

SIKU ZA MWANZO

Hazrat Abubakar (ra) alizaliwa katika mji wa kale wa Maka ilipo Kaaba (nyumba ya kwanza kwa ajili ya kumuabudu Allah). Maka pia ndipo alipozaliwa Mtukufu Mtume Muhammad (saw). Wote wawili walitokana na kabila la Qureishi. Ingawaje hatufahamu kwa uhakika lini Hazrat Abubakar (ra) alizaliwa, lakini tunachoelewa alikuwa mdogo kwa Mtukufu Mtume (saw) kwa miaka miwili na nusu hadi mitatu.

Baba yake alikuwa Uthmani Abu Quhafah pia aliitwa Abu Quhafa na Mama yake aliitwa Umul Khair Salma wote walikuwa ukoo wa Bani-Tamiim kabila la Waqureishi. Alipozaliwa Abubakar alipewa jina Abdul qa’aba (mtumishi wa kaaba) lakini baada ya kupokea uislamu Mtukufu Mtume Muhammad[sawa] aliligeuza na kumuita Abdullah (mtumishi wa Allah) kwa sababu ya unyoofu wa hulka yake na uzuri wa sura watu walimuita al
Ki. Kwasababu alikuwa mwanaume wa kwanza kuingia katika uislamu akajulikana kama Suddiq (mkweli).

Ni kwa masikitiko ya kwamba atujui mengi kuhusu historia ya utoto wake. Alikuwa ni Rafiki wa karibu wa Mtukufu mtume. [sawa] Alifariki akiwa na umri uleule wa mtukufu mtume [saw.]

3

MFANYABIASHARA TAJIRI NA HAKIMU MWADILIFU.

Kabla ya kupokea Islam Hadhrat Abubakarira alikuwa mfanyabiashara na alikuwa na desturi ya kwenda Syria na Yemeni katika safari zake za kibiashara. Safari yake ya kwanza ya kibiashara ni wakati alipokuwa na umri miaka kumi na nane na baada ya miaka michache akawa mfanyabiashara maarufu na Tajiri wa Makka. Wale walioishi Makka na nje ya Makka waliofanyabiashara nae walimpenda sana na kumuheshimu kwajili ya uaminifu wake, hekima, hulka njema na ushauri ulio mzuri. Hakuna aliyeelewa koo na historia za kabila la kikureishi kama Hadhrat Abubakari Swiddik. Mara kwa mara uhasama ulipofumuka miongoni mwa makureishi Hadhrat Abubakarira aliitwa kuwa mpatanishi.

4

WA KWANZA KUAMINI

Mtukufu mtume saw alipokuwa tangaza kuwa Mtume Hadhrat Abubakari ra alikuwa nje kidogo Ya mji wa Makka. Mara tu baada ya kurudi viongozi wakubwa wa Makka wakiwemo Amir bin Hisham (Abu Jahl) na Shaibah walimtembelea na wakamwambia kwa kebehi kwamba mpwaye Abu Twarib amedaai kuwa yeye ni mtume.

Baada ya mazungumzo hayo na hao mabwenyenye wa makka alikwenda moja kwa moja kwa Mtume Muhammad [saw] na akamuhuliza kama amedai kuwa mtume kutoka kwa allah. Mtume Mtukufu alianza kutoa maelezo lakini Hadhrat Abubakari ra alimkatisha na akamuuliza tena kama amedai kuwa Mtume wa Allah. Mtukufu Mtume Muhammad [saw] alijibu kuwa ni kweli ameteuliwa kuwa Mtume wa Allah sw mara tu baada ya kusema hivyo Hadhrat Abubakari ra kwa haraka alisema ninashuhudia kuwa wewe ni Mtume wa Allah sw.

Kwasababu hiyo Hadhrat Abubakari ra anahesabiwa kuwa miongoni mwa wale Waislamu kuwa watu wa nyumba ya Mtume ambao ni Pamoja na Hadhrat Khadija ra, Hadhrat alli ra na mtumwa aliyewekwa huru wa Mtukufu Mtume saw Hadhrat Zahid bin haris ra. Kukubali moja kwa moja Islamu Hadhrat Abubakar ra kunadhihilisha Imani yake thabiti kwa Mtume Muhammad [saw] kwani alijuwa kuwa daima Mtukufu Mtume Muhammad saw alikuwa mkweli. Kuna siku Mtume saw alipokuwa anazungumzia Sayyidna Abubakar ra kila mmoja niliyemfikishia mafundisho ya Islamu alisita kabla ya Muislamu isipokuwa Hadhrat Abubakari ra ambaye mara moja alikubali Islamu bila ya shaka yoyote.

JINSI YA KUTENGENEZA ICE CREAM BILA YA KUTUMIA MASHINE

Vitu vya kuandaa.

1. Maziwa ml 240
2. Sukari ml 240
3. Chumvi kijiko kidogo cha chai robo (1/4)
4. Vanilla ya maji kijiko kikubwa cha chakula 1/2
5. Vanilla ya mti ml 120
6. Low fat maziwa ml 120
7. low fat cream ml 120
8. Whipping cream yenye ubaridi wa wastan ml 480
9. Biskuti zilizochovywa Chocolate 10 cream ml 480

Badala ya biskuti zilizochovywa na chocolate cream unaweza weka vipande vya chocolate, unaweza weka mchanganyiko wa ladha mabalimabli mfano matunda kama strawbery, cherry, Embe kwa kuchanganya kiasi cha ml 480 kama inavyoonyehs hapo juu katika mtiririko wa vitu vya kuandaa.

Vunja vunja vipande vya biscuti vilivyochovywa na chocolate weka pembeni safi ukisubiri baadae kidogo kuzitumia.

Weka maziwa katika sufuria nzito kwenye jiko lenye moto wa wastan acha yachemke pole pole mpaka yatakapotoa mapovu pemebi ya sufuria yatoe na weka pembeni yapoe.

Baada ya kutoa maziwa katika moto na kuyaweka pembeni yapoe changanya sukari na chumvi ndani yake

Koroga vizuri maziwa hayo mpaka sukari na chumvi viyeyuke vizuri

Changanya tena whiping cream na vanillah kwenye maziwa yale pole pole kisha changanya maziwa na ile cream vilivybaki ambavyo vyote vinamafuta kiasi (low fat) mpaka ichanganyike vizuri.

Kisha mimina mchanganyiko wako wote kwenye bakuli safi la kioo ili uweze kupoa na kuganda

Baada ya kumimina katika bakuli chukua bakuli jingine kubwa kiasi ya lile lenye mchanganyiko wako kwajili ya kugandisha kua ice cream. Weka barafu katika bakuli hilo kisha weka juu yake bakuli lenye mchanganyiko wako. Baada ya mchanganyiko wako

kupoa kabisa chukua plastic wrap funika bakuli lako vizuri na weka katika friji kwa masaa 4 au hata masaa 24 kwa
kuweka mchanganyijo wako ndani ya friji itasaidia sana kubadilisha mchanganyiko kua rojo rojo au mzito na inakua rahisi kukoroga tena ili upate umbile halisi la ice cream na laini kwa mlaji.

Baada ya masaa 4 au masaa 24 toa mchanganyiko wako kwenye friji kisha koroga vizuri na mwikosafi wa mbao au kijiko kikubwa.

Kisha funika tena na plastic wrap au foil kitu chochote kitakachozui hewa kuingia katika bakuli lako tayari kwa kugandisha kwenye freezer. Baada ya hapo weka bakuli lako katika freezer na ruhusu mchanganyiko wako ukae kwa masaa 2 kwenye freezer kisha utoe.

Baada ya kutoa mchanganyiko wako katika freezer tumia mashine ya kuchapia au unaweza tumia mchapo wa chuma au unaweza tumia uma ya kulia chakula na kukoroga vizuri mchanganyiko amabao utakua tayari umeshaanza kuganda lengo ni kuvunjavunja mapande ambayo yameshaanza kuganda. Kisha funika na plastic wraptena na rudisha katika freezer kwa masaa 2.

Baada ya masaa 2 toa mchanganyiko wako na koroga kwa kutumia mashine au uma yakulia chakula. Ice cream yako itakua nzito safi lakini bado kwa kuweza kuchota na kuliwa, kama mchanganyiko bado haujaganda vizuri kutokana na nguvu ya freezer rudisha kwenye freezer igande tena kwa muda kiasi.

Baada ya ice cream yako kua imeganda vizuri chukua zile bisckuti zenye chocolate tupia katika mchanganyiko wako wa ice cream na uchanganye vizuri sana kwa umakini, aidha inaweza kua ni matunda ya ladha yeyote badala ya biskuti bado itapendeza na utakua umebadilisha ladha.

Kisha funika vizuri plastic yako na mfuniko safi na uirudishe katika freezer iweze kuganda kabisa mpaka itakapokua ngumu.

Baada ya ice cream kua ngumu toa kwenye freezer fungua chombo chako cha plastik na tumia chombo maalumu cha kuchotea ice cream vipo vingi sana hapa nyumbani tanzania vinauzwa kwenye supermaket. Chota maumbo mazuri sana ya mviringo kisha weka kwenye bakuli au glasi ya udongo na ufurahie ice cream yako!

KUTOKA MAKTABA

Mzee Rashid Msabaha - Sehemu ya II

KUJIUNGA NA JAMAAT.

Kujiunga kwake na Jumuiya kunanasibishwa na njozi aliyoota.

Alikuwa amekwenda katika msitu wa Jangwani (enzi hizo Jangwani ni pori kubwa) kwa ajili ya kutafuta Uwalii. (Daraja la kiroho katika Dini ya Islam).

Huko, alijitenga kwa siku kadhaa akifunga, kusali na kufanya maombi mbalimbali.

Siku moja akapata njozi. Katika njozi alijiona yuko pamoja na masheikh wake, yaani Sheikh Idrisa na Sheikh Hashir. Mara kitu fulani chenye nuru kiliteremka kutoka mbinguni kikamfunika. Akawa anawafuata Masheikh wake huku akiwa amefunikwa na kile kitu chenye nuru. Ajabu kila akiwafuata, Masheikh wake wakawa wanamkimbia. (mwisho wa njozi)

Aliporudi kutoka Jangwani akamhadithia Sheikh Idrisa njozi yake. Sheikh hakujua taawili ya njozi ile. Akamshauri atafute kitabu cha tafsiri za ndoto kiitwacho *Ta'atirul Anaam.* Humo hakupata tafsiri ya njozi yake. Sheikh akamwambia tena atafute kitabu kingine kinaitwa *Maashallah.* Humo pia tafsiri haikupatikana. Basi njozi ikaendelea kumsumbua huku akiuliza hapa na pale nini maana yake.

Siku moja akakutana na Sheikh Kaluta Amri Abedi akiwa anahubiri Kariakoo, akamuhadithia na kisha akamuuliiza iwapo anafahamu tafsiri ya njozi yake.

Sheikh Amri Abedi akamwambia afuatane nae hadi msikitini kwa sheikh Mubarak Ahmad. Sheikh Mubaraka akamtafsiria njozi yake kuwa, utapokea nuru ambayo ni ujumbe wa Allah.

Nuru yenyewe ni Mtume wa Allah aliyedhihiri zama hizi naye ni Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] ambaye ndiye mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya. Sheikh Mubarak akachukua kitabu kilichokuwa imeandika Hotuba maarufu ya Hadhrat Ahmad a.s 'Khutba Ilhaamiyya' akamsomea maneno yasemayo *"wa anaa dhaalika Nuur..".* yakielezea kuwa, Hadhrat Ahmad[as] ndio hiyo Nuru …".

Taawili aliyopewa na maneno hayo yakamuathiri roho na moyo wake, hakuwa na budi isipokuwa kumkubali mjumbe wa Allah na kujiunga na Jamaat.

Alipeleka habari kwa Masheikh wake juu ya taawili ya njozi yake na kumfahamisha kuwa amemtambua Imam wa zama na amejiunga na Jumuiya ya Ahmadiyya.

Sheikh Idrisa akamwambia wewe umeisha tanassar yaani umetoka nje ya Islam.

Akawaendea wanafunzi wenzake kuwapa habari hiyo, nao wakamkimbia!.

Njozi ikatimia barabara. *Itaendele inshallah*

MAHUBIRI KATIKA MJI WA BAGAMOYO

Kutoka uk. 4

Alitoa shukran kwa Majlis Ansarullah kwa kusema kuwa, wao wameonesha njia kwa kuja na wazo hili na Khuddamul Ahmadiyya wataendelea kuunga mkono kwa kushiriki kwa hali na mali kwa sababu lengo la Tanzim hizi ni moja la kuhakikisha Ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa (as) na ujumbe wa Islam unawafikia watu wote duniani.

Aidha aliwashukuru kamati iliyohusika kwa maandalizi mazuri ya shughuli nzima na wale wote waliojitolea mali zao katika kufanikisha Mahubiri hayo.

Baada ya hapo, Sadr Ansarullah na Sadr Khuddam, walitoa tamtam kwa Atfal wote ili kuwatia moyo na kuwahamasisha kushiriki shughuli za Jamaat.

Na mwisho, ilipigwa picha ya pamoja na Sadr Khuddam aliongoza maombi na tayari kwa kuondoka kurudi Dar es salaam.

Safari ya kurejea ilianza rasmi majira ya saa moja kamili magharibi watu wote wakiwa na furaha na kuridhika kwa kile walichotekeleza.

Ikumbukwe kwamba, shughuli hii ya mahubiri na Picnic, imefanyika kama shamrashamra za kuelekea kilele cha maadimisho ya Siku ya Mwana Aliyeahidiwa

Tunamuomba Allah Ajaalie tabligh hiyo ilete matunda bora na pia Ajaalie maadhimisho mema ya siku ya Mwana Aliyeahidiwa ambayo huuadhimishwa kila tarehe 20 Februari ya kila mwaka.

Neno letu la mwisho, ni Kila sifa njema anastahiki Allah Mola wa walimwengu.

MATUKIO KATIKA PICHA





Matukio mbalimbali jinsi mkoa wa Dar es salaam walivyoanzimisha Siku ya Mwana aliyeahidiwa







Siku ya Mwana aliyeahidiwa ilivyoazimshwa Bariadi



Siku ya Mwana aliyeahidiwa Unguja (ZNZ)



Maadhimisho ya mwana aliyeahidiwa Mbeya



Siku ya Mwana aliyeahidiwa Makao Makuu ya Nchi Dodoma.



Chuo cha Jamia Morogoro chaazimisha Siku ya Mwana aliyeahidiwa.





Matukio mbalimbali ya Mahubiri ya PICNIC Bagamoyo katika kuazimisha siku ya Mwana aliyeahidiwa.

MAPENZI YA SEYDNA AHMAD KWA MTUME S.A.W.

Kutoka uk. 1

Tafsiri: Sema, kama baba zenu, na wana wenu, na ndugu zenu, na wake zenu, na jamaa zenu, na mali mlizochuma, na biashara mnazoogopa kusimama, na majumba mnayoyapenda ni vipenzi Zaidi kwenu kuliko Allah na Mtume Wake na kufanya juhudi katika njia Yake, basi ngojeni mpaka Allah Alete amri Yake, na Allah Hawaongozi watu waasi.

Ukweli ndio huu kwamba, upendo wa seyyedna Ahmad as. kwa Bwana wake ulikuwa kiini cha roho yake na uzima wake, matukio mbali mbali, yapendezayo yaliyojaa mapenzi, mahaba na utii usio wa kwaida, yanaonekana maishani mwake kiasi hiki kwamba mtu anapigwa na bumbuwazi.

Masharti na vigezo vyote vya mapenzi ya kweli vina hakiki katika kila secunde ya maisha yake, ambayo yananga'a na mifano ya aina hii kama mbingu inavyonga'a kwa nyota mbali mbali. Naweza kusema kwa haki kwamba jinsi Seyidna Ahmad a.s. alivyompenda Mtume (s.a.w.) kakuna mwingine awezaye kujifananisha naye, wala upendo wake kwa Mtume (s.a.w) haune mfano katika historia yote ya Kiislam. Mtu yoyote hawezi kupinga kauli hii kuwa: daraja na makamu ya Seyidna Ahmad a.s. katika kumpenda Mtume (s.a.w) iko juu zaidi hata kuliko akili na fahamu ya watu.Wallahi! mapenzi na Ikhlasi yake kwa mtume (s.a.w) haina mwisho wake,na ni kama bahari isiyo na mipaka.Tunapata harufu za mapenzi yake kwa bwana wake kutoka katika kila neno la maandishi yake, tunaona wazi aksi ya uzuri wa Mtume (s.a.w) kwenye mwenendo na tabia ya Seyidna Ahmad a.s. tunashuhudia jazba yake ya kudumu ya kujitolea muhanga kwa heshima na taadhima ya Mtume (s.a.w) kwenye kila nia na mpango wake.

Tangazo zuri lilioje la mapenzi na mahaba!

جِسْمِی یَطِیرُاِلَیکَ مِن شَوقٍ عَلا۔ یَا لَیتَ کَانَت قُوَّۃُ الطَّیرَانِ

idiaz eyadnepma eyidn uyuh inaay .(w.a.s) emutM

in uuh !ijamosaw ugnaz ugudN izeynewM an awelotoilu aduhuhsu ekaw onafm anuah oabma ,ugnuM awK .malsiik ay etoy airotsih akitak awas awas in uuh odnepu ilewk ugnuM izeynewM ay iih irma an oyamesi: اِنْ کُنْتُمْ تُحِبُّوْنَ اللّٰہَ فَاتَّبِعُوْنِیْ یُحْبِبْکُمُ اللّٰہُ قُلْ (23:3)

adnepmawm iynin awiki :ameS hallA ,inetaufin isab ,hallA …inednepawatA

utaw aw aduhuhsu aotikiN

wasiokuwa waislam, ningependa kuweka mbele yenu maneno ya Babu Muhammed Athmaan wa Lakhnau naye alisema kwamba:- Yeye alienda Qadian mnamo mwaka 1918 na kuonana na Mbaniani mmoja aitwaye Lala Malawamal au Lala Budhamal na kumuuliza kuwa unamuonaje Mirza sahib, kwani wewe ulimuona tangu umri wake mdogo ? Mbaniani huyo akajibu :-

"Sijawahi kumuona mwislamu yeyote, mwenye kumpenda Nabii wake zaidi kuliko Mirza Sahib ''.

Hadhrat Dr. Mir. Mohammed Ismaail sahib akitoa ushuhuda wake wa binafsi alisema:- Ninasema kwa kuapa kwa jina la Allah kuwa, sijamuona yeyote aliyezama katika mapenzi ya Allah na ya Mtume Muhammad (S.a.w) zaidi kuliko Mirza Sahib.

Alama moja wapo ya mapenzi ya kweli ni kwamba Aashiqi humkumbuka mpendwa wake muda wote. Seyyidnaa Ahmad (a.s) kutokana na maarifa ya kuitambua shani adhimu ya Mtume (s.a.w) aliyojaaliwa na Mwenyezi Mungu, aliujaza moyo wake safi kwa mapenzi ya Mtume Muhammad (s.a.w) kiasi hiki kwamba, alimkumbuka bwana wake usiku na mchana akimsalia na kumtakia rehema, akieleza hali yake hiyo alisema katika ubeti wake mmoja wa kiarabu kuwa:

ذِکْرُ الْمُصْطَفٰی رُوْحٌ لِقَلْبِیْ ۔ وَصَارَ لِمُهْجَتِیْ مِثْلَ الطَّعَامِ

"kumkumbuka Mtume (s.a.w) ni kiini cha moyo wangu na chakula cha mwili wangu ambacho ni sababu ya uhai wangu."

pia alisema katika ubeti wa kiurdu kwamba:

ربط ہے جانِ محمد سے میری جاں کو مدام۔ دِل کو وہ جام لَبالَب ہے پلایا ہم نے

Roho yangu inauhusiano imara wenye kudumu na roho ya Mtume (s.a.w) na tumeunywesha moyo wetu kinywaji hiki cha upendo kwa wingi :

Hadhrat Shiekh Yukub Ali Irfani Sahib anasimuliwa kuwa nilipoenda Uengereza mnamo mwaka 1925 niliwahi kuonana na Padre Dr. White Braikht ambaye aliyekuwa Missionary katika mji wa Batala naye alionana na Seyyidnaa Ahmad (a.s) mara kadhaa. Sheikh Sahib anahadihtia kuwa Padre huyu alisema: Mimi nilishuhudia jambo moja katika tabia ya Mirza Sahib, ambalo sikulipenda nalo ni kuwa: kila mara aliposingiziwa (Mtume s.a.w) basi Mirza Sahib alikasirika na rangi ya uso wake ulikuwa unabadilika na kuwa mwekundu. Hadhrat Yakub Irfani Sahib alimjibu: Padre Sahib jambo linalokuchukiza ndilo linalotupendeza sisi zaidi. (unalolichukia ndilo tunalipenda)

Sisi twajua ya kuwa Seyidna Ahmad a.s alipata mashaka mengi maishani, alipata mateso makali, aliona misiba ya jamaa wengi miongoni mwa watoto na ndugu na marafiki na alionja machungu mengi; lakini maudhi hayo yote na shida nyingi mno alizozipata hazikuweza kumfanya alie juu ya hasara zake. Ni uchungu mkubwa ulioje wa kukumbuka kifo cha Bwana wake faraghani kilichotokea miaka Zaidi ya 1,300 uliomfanya alie machozi aliposoma utenzi wa mahaba uliotaja hasara ya kupotea kwake Mtume Muhammad s.a.w. duniani! katika maisha yake mtu anakabiliwa shida nyingi. Penginie anafiwa na wazazi. Pengine watoto wanakufa. Pengine mume au mke anakufa. Ni mazito sana hayo yote mwanadamu kuyavumilia. Lakini siku zinapozidi kupita majeraha hayo yanapona pole pole mpaka mtu anasahau maumivu yake. Ni makubwa yalioje mapenzi ya huyu mtumishi juu ya Bwana wake ambaye akimkumbuka msiba wake baada ya miaka 1,300, macho yake yanatiriri sha machozi kama mvua kana kwamba kifo chake kimetokea leo. Jeraha la moyoni mwake halikupona ingawa zilipita karne 13.

Hapa nataka kuwaambia ndugu zangu Waislamu ambao hadi sasa hawajawa na bahati ya kujiunga na Jumuiya ya Ahmadiyya na kusaidiana nasi katika huduma ya kuuhami Uislamu ya kwamba wao wafikirie tukio hili tu peke huku wakimwogopa Mwenyezi Mungu. Je, mtu wa namna hii anaweza kutoka nje ya kundi la wafuasi wa Mtume s.a.w.?

kisha Seyyedna a.s. anasema katika shaairi lake la kiajemi kuwa:

Katika mwili wa Mtume s.a.w. Mwenyezi Mungu ameweka nuru ya ajabu na chimbo lake takatifu limejaa majohari na maalmasi ya fahari, Basi enyi wenye kiburi, ikiwa mnatafuta hoja ya ukweli wake, ingieni katika wafuasi wake, maana dhati yake yenyewe ni hoja kubwa ya ukweli wake. Wallahi kama mimi nikatwe vipande vipande katika njia hii na chembe chembe zote za mwili wangu zichomwe moto na kugeuka kuwa majivu, mimi sitaondoka mlangoni pake. Ewe nafsi ya Mtume, nafsi yangu iwe sadaka kwako! Mapenzi yako yameangaza mwili wangu wote.

(Aaina e kamalat e Islam)

Seyyedna Ahmad as aliandika akieleza nuru ilyopatikana katika nafsi tukufu ya Mtume saw kwamba:

Nuru ile ya hali ya juu aliyojaaliwa mwanadamu, yaani mwanadamu mkamilifu, hawakujaaliwa malaika, wala nyota, wala mwezi, wala jua, wala haikuwemo baharini na mitoni, wala haikupatikana katika lulu, yakuti, zumaridi na almaasi. Ilimuraadi hakuna kitu cho chote cha ardhini au mbinguni kilicho jaaliwa hiyo nuru isipokuwa mwanadamu mkamilifu, ambaye mfano wake kamili, na wa hali ya juu sana ni Mtume Muhammad (s.a.w) aliye bwana wetu, kiongozi wetu, fahari wa manabii wote na mbora wa viumbe .

Wasomaji wapendwa! ni nani anaeweza kusahau lile tukio maarufu lililobeba ushuhuda wa malaika ambapo Seyidna Ahmad a.s. aliona katika ru'uiya, malaika walileta mitungi ya nuru nyumbani kwa Seyidna Ahmad a.s na mmoja wao akisema:

"هٰذَا بِمَاصَلَّیْتَ عَلٰی مُحَمَّدٍ"

(Hakikatul Wahi, Rohani Khazain J.22 uk.131, mapimbizo)

yaani hizi ni baraka zako za kumsalia na kumtakia rehma Mtume s.a.w.

Matokeo ya lazima ya mapenzi ni mtu kutaka kujitoa mhanga nafsi yake kwa ajili ya mpendwa wake na kuwa na ghera juu yake. Haiwezekani mtu kukosa ghera kwa ajili ya mpenzi wake au kukosa nia ya kujitoa maisha yake kwa ajili yake.

Seyyidna Ahmad a.s. anasema akituelezea Baraka za kumfuata mtume s.a.w.kwa kutaja kabisa dhati yake yeye mwenyewe kuwa:

"Isingeliwezekana kwangu mimi kuipata neema hii kama nisingefuata nyayo za Bwana kiongozi wangu, fahari ya Manabii wote, Mbora wa wanadamu, Muhammad, Mteule, amani na baraka za Mungu ziwe juu yake. Mafanikio yo yote nimeyapata kwa kumfuata yeye, nami najua kutokana na uzoefu uliohakiki, ya kwamba hapana awezeye kumpata Mwenyezi Mungu na kupata elimu ya ndani ya njia zake bila kumfuata Nabii huyu, amani na baraka za Mungu ziwe juu yake."

Seyidna Ahmad a.s. alikuwa na sifa hizi kwa ukamilifu kwa ajili ya Kiongozi wake na Bwana wake, Mtume Muhammad s.a.w. akitaja masingizio ya Wakristo wanayoleta juu ya nafsi takatifu ya Mtume s.a.w. amesema: "Mapadre wa Kikristo wamezua mengi juu ya Mtume wetu s.a.w Hakuna kitu kilichoniudhi roho yangu zaidi kuliko hayo maneno ya dhihaka na maskhara wanayotunga wao juu ya mtakatifu Mtume wetu huyu. Moyo wangu umejeruhika kwa sababu ya hao kumkashifu na kumwaibisha mbora wa viumbe. Anasema;

"Haki ya Mungu, kama watoto wangu wote na wajukuu wangu na vilembwe wangu na marafiki zangu na wasaidizi wangu wote wauawe mbele ya macho yangu, hata mimi mwenyewe nikatwe mikono na miguu, na mboni za macho yangu kutolewa nje, wala nisipate mradi wangu hata moja, tena ni nyimwe furaha na starehe zangu zote, shida hizi zote si kitu zikilinganishwa na msiba wa Mtume s.a.w. kufanyiwa mashambulio machafu. Ee Mola wetu uliye mbinguni! Utuhurumie na kusaidia na kutuokoa na mtihani huu mkubwa."

Je, ghera ya namna hii, mfano wake waweza kupatikana kwa mwislamu yeyote au mahali pengine popote katika zama hizi?

Inaendelea uk. 11

MAPENZI YA SEYDNA AHMAD KWA MTUME S.A.W.

Kutoka uk. 10

Je, mapenzi kama haya yaweza kuonyesha katika mtu mwingine hivi sasa?
Hayo siyo madai matupu, bali kila tukio la maisha ya Seyidna Ahmad a.s liwe kubwa au ndogo, linatoa ushahidi juu ya mapenzi hayo hayo.

Mnamo mwaka 1893 Seyidna Ahmad a.s. alifanya mjadala na Wakristo wa Mji wa Amritsar, mjadala huu ulisha chapishwa kwa jina la vita tukuf (Jange Mukaddas) Dr. Padre Martin Clark ambaye alikuwa mkuu wa Wakiristo alimwalika Seyidna Ahmad a.s. pamoja na baadhi ya Masahaba zake kwenye chai.

Seyidna Ahmad a.s. hakukubali mwaliko wake kwa sababu hii tu kwamba, hawa watu wanamvunjia heshima Mtume s.a.w. basi hatuwezi kukubali mwaliko wao na kukaa nao isipokuwa kwa ajili ya kubadilisha itikadi zao za uwongo.

Hali kadhalika, Seyidna Ahmad a.s. alipofanya mjadala na Padre Deputy Abdallah Atham, siku zile zilikuwa za joto kali sana na kila mtu alikuwa anapatwa na kiuu mara kwa mara na maji ya kunywa yalikuwa yanahitajika sana na mahali pa jirani kulikuwa na kisima cha maji baridi cha Wakristo lakini Seyidna Ahmad a.s. hakupenda kuchukuwa maji kutoka kwao kutokana na shutuma zao dhidi ya Mtume s.a.w. Tukio hili linaonesha mahaba na ghera yake kwa Mtume s.a.w.

Mtukio hayo ni dalili bayana juu ya mapenzi yake kwa Bwana wake Mtukufu Mtume Muhammad jinsi ilivyobainishwa ndani ya kauli ifuatayo ya Mtume saw kwamba:
حَدَّثَنَا يَعْقُوبُ بْنُ إِبْرَاهِيمَ ، قَالَ: حَدَّثَنَا ابْنُ عُلَيَّةَ ، عَنْ عَبْدِ الْعَزِيزِ بْنِ صُهَيْبٍ ، عَنْ أَنَسٍ ، عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ. ح وحَدَّثَنَا آدَمُ ، قَالَ: حَدَّثَنَا شُعْبَةُ ، عَنْ قَتَادَةَ ، عَنْ أَنَسٍ ، قَالَ: قَالَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: لَا يُؤْمِنُ أَحَدُكُمْ حَتَّى أَكُونَ أَحَبَّ إِلَيْهِ مِنْ وَالِدِهِ وَوَلَدِهِ وَالنَّاسِ أَجْمَعِينَ .
(Sahih Bukhari Kitabul Iman Hadithi no.15)
Tafsiri: imesimuliwa na hazrat Anas r.a.kwamba mjumbe wa Allah saw alisema: hawezi mmoja wenu awe Mu'mini mpaka anipende mimi Zaidi kuliko wazazi wake, Watoto wake na watu wengine wote.

Siku moja Seyidna Ahmad a.s. alikuwa amekaa ndani ya chumba chake pamoja na Masahaba zake na wageni wengine, mtu mmoja aligonga mlango wake na sahaba mmoja alitaka kumfungulia mlango, lakini Seyidna Ahmad a.s. aliharakia kwenda kwenye mlango akimwambia sahaba wake subiri subiri, ninafungua mlango mimi mwenyewe kwani wewe ni mgeni na bwana wetu Mtukufu ameagiza kwa ajili ya kumkarimu mgeni.

Kila makala aliyoandika na kila shairi alilotunga juu ya mtume s.a.w. limefanana na shimo refu lenye kina kirefu lililojaa almasi na lulu za mapenzi ya mtume s.a.w. zisizo na kikomo.

Binti mkubwa wa Seyidna Ahmad a.s. Hadhrat Nawab Mubaraka Begam, ambaye pia ni mmoja wa watoto waliotabiriwa kuzaliwa kwa Sedna Ahmad a.s ambaye ni mwenye busara nyingi na akili pevu, anasimulia hivi ; "Siku moja Seyidna Ahmad a.s. alikuwa hajisikii vizuri na alikuwa amelala kitandani na mama na Hadhrat Mir Nasir Nawab (babu mzaa mama) vile vile walikuwa wamekaa karibu naye, mara yakatokea mazungumzo juu ya Haji.

Hadhrat Mir Nasir Nawab alisema ya kuwa sasa njia ya kwenda kuhiji imerahisika kidogo na ni afadhali mtu afanye Haji katika siku hizi hizi. Kwa kukumbuka hivi Makka na Madina, mahali patakatifu pa Uislamu, macho ya Seyidna Ahmad a.s. yakajaa machozi naye akawa anayafuta kwa kidole chake, kasha akasema; "Ni kweli na mimi pia natamani kuhiji; lakini mara nyingi hufikiri nikifika Madina, je nitaweza kujizuia nitakapotazama kaburi la Mtume s.a.w?"

Hazrat Ahmad a.s. anasema katika shairi lake la kiajemi kuwa:
" بعد از خدا بعشقِ محمد مخمّرم۔ گر کفر ایں بوَد بخدا سخت کافِرَم"
yaani Nimejilevya kikamilifu na mapenzi ya Mtume Muhammad (s.a.w) baada ya mapenzi ya Mwenyezi Mungu, kama hiyo ni kufuru basi wallaahi mimi ni kafiri mkubwa sana.

Wasomaji watukufu, bila shaka yeyote ubeti huu hauna mfano wake katika ulimwengu wa mapenzi na mahaba.

Halafu pengine anasema:
"Daima nastaajabia sana Nabii huyu Mwarabu, aitwaye Muhammad, maelfu ya baraka na amani view juu yake. Cheo chake cha juu kilioje? Haiwezikani kujua upeo wa daraja la hali ya juu, mwanadamu hawezi kufahamu vina na unduni wa athari ya khulka zake zilizotukuka. Yasikitisha daraja lake lililonyanyuka sana halikufahamika vyema.

Ule umoja wa Mungu uliokuwa umetoweka duniani ukafufuliwa tena na huyu mshindi mkuu. Alimpenda Mwenyezi Mungu kwa mapenzi ya kupindukia, na kujitaabisha kwa kuwahurumia wanadamu.

Ndio maana Mwenyezi Mungu, aliyemjuzi wa siri ya moyo wake, akamfadhili zaidi kuliko Manabii wote na watu wote wa zamani na wale watakaokuja baadaye, na akamtimizia matakwa ya moyo wake katika uhai wake."
(Roohani Khazain Jal. 22: Hakikatul- Wahy Uk.116-115).
Maandishi yafuatayo pia hayana mfano, Hazrat Ahmad a.s.anasema:
"Tuchunguzapo kwa roho safi bila mapendeleo Nanabii wote wa zamani, twapata ya kwamba Hadhrat Muhammad mtume Mtukufu wa Kila makala aliyoandika na kila shairi alilotunga juu ya mtume s.a.w. limefanana na shimo refu lenye kina kirefu lililojaa almasi na lulu za mapenzi ya mtume s.a.w. zisizo na kikomo.

Binti mkubwa wa Seyidna Ahmad a.s. Hadhrat Nawab Mubaraka Begam, ambaye pia ni mmoja wa watoto waliotabiriwa kuzaliwa kwa Sedna Ahmad a.s ambaye ni mwenye busara nyingi na akili pevu, anasimulia hivi ; "Siku moja Seyidna Ahmad a.s. alikuwa hajisikii vizuri na alikuwa amelala kitandani na mama na Hadhrat Mir Nasir Nawab (babu mzaa mama) vile vile walikuwa wamekaa karibu naye, mara yakatokea mazungumzo juu ya Haji.

Hadhrat Mir Nasir Nawab alisema ya kuwa sasa njia ya kwenda kuhiji imerahisika kidogo na ni afadhali mtu afanye Haji katika siku hizi hizi. Kwa kukumbuka hivi Makka na Madina, mahali patakatifu pa Uislamu, macho ya Seyidna Ahmad a.s. yakajaa machozi naye akawa anayafuta kwa kidole chake, kasha akasema; "Ni kweli na mimi pia natamani kuhiji; lakini mara nyingi hufikiri nikifika Madina, je nitaweza kujizuia nitakapotazama kaburi la Mtume s.a.w?"

Hazrat Ahmad a.s. anasema katika shairi lake la kiajemi kuwa:
" بعد از خدا بعشقِ محمد مخمّرم۔ گر کفر ایں بوَد بخدا سخت کافِرَم"
yaani Nimejilevya kikamilifu na mapenzi ya Mtume Muhammad (s.a.w) baada ya mapenzi ya Mwenyezi Mungu, kama hiyo ni kufuru basi wallaahi mimi ni kafiri mkubwa sana.

Wasomaji watukufu, bila shaka yeyote ubeti huu hauna mfano wake katika ulimwengu wa mapenzi na mahaba.
Halafu pengine anasema:
"Daima nastaajabia sana Nabii huyu Mwarabu, aitwaye Muhammad, maelfu ya baraka na amani view juu yake. Cheo chake cha juu kilioje? Haiwezikani kujua upeo wa daraja la hali ya juu, mwanadamu hawezi kufahamu vina na unduni wa athari ya khulka zake zilizotukuka.
Yasikitisha daraja lake lililonyanyuka sana halikufahamika vyema. Ule umoja wa Mungu uliokuwa umetoweka duniani ukafufuliwa tena na huyu mshindi mkuu. Alimpenda Mwenyezi Mungu kwa mapenzi ya kupindukia, na kujitaabisha kwa kuwahurumia wanadamu. Ndio maana Mwenyezi Mungu, aliyemjuzi wa siri ya moyo wake, akamfadhili zaidi kuliko Manabii wote na watu wote wa zamani na wale watakaokuja baadaye, na akamtimizia matakwa ya moyo wake katika uhai wake."
(Roohani Khazain Jal. 22: Hakikatul-Wahy Uk.116-115).

Maandishi yafuatayo pia hayana mfano, Hazrat Ahmad a.s.anasema:
"Tuchunguzapo kwa roho safi bila mapendeleo Nanabii wote wa zamani, twapata ya kwamba Hadhrat Muhammad mtume Mtukufu wa Islam (s.a.w.) ndiye shujaa kupita wote, ndiye aliyekusanya sifa zote za maisha na ndiye aliyempenda Mwenyezi Mungu zaidi."
(Roohani khazain Jal. 12: Siraje-e-Muneer Uk. 72)

Ningependa kumaliza madhumuni yangu kwa maneno haya ya Seyidna Ahmad a.s. yeye anasema:
Hapana mtume wala mwombezi kwa ajili ya wanadamu, ila mtume Muhammad s.a.w.kwa hiyo jitahidini mumpende kwa mapenzi kweli kweli mtume huyu, mtume wa heshima na utukufu.

Na wala msimheshimu mtu yeyote kuliko yeye ili mwandikiwe mbinguni miongoni mwa wale waliookoka.

E, Mola wetu! Umrehemu,Umbariki na kumneemesha Mtume wetu na wafuasi wake kama Ulivyombariki Ibrahim na ahali zake na Utuwezeshe kumpenda Mtume Wako jinsi alivyompenda Aashiki wake na kutujalia na baraka zote za kumfuata na kumtii nabii huyu adhimu.Aamin.
(Sheikh Karim Uddin Shams. Mbeya)

Itaendelea toleo Lijalo

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

MapenziyaMungu

JAM.II -RAJAB.1443 AH | MARCH 2022 | TABLIGH 1401 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufusaw

Imesimuliwa na Hadhrat Ibn Mas'ud r.a. ya kwamba Mjumbe wa Allahsaw alisema: Mkiwa watatu, basi wawili kati yenu wasinong'onezane kwa kumwacha yule wa tatu mpaka mchanganyike na watu, kwani jambo hilo litamhuzunisha huyo (**Muslim**).

Upendo wa Ahmad as. Kwa Mwenyezi Mungu



Na jambo linalotakiwa kutajwa mwanzoni kabisa ni Mapenzi ya Mungu, maana ni
kiungo imara kabisa baina ya mtu na Muumba wake. Tunapoangalia Maisha ya Seyyidna Ahmad a.s. tunapata yakini kamili kuwa yeye alikuwa anampenda Mola wake kwa kiasi kikubwa sana na alitumia kila
dakika ya maisha yake katika kumkumbuka Mwenyezi Mungu.
Na mapenzi yake kwa Mola wake yalikuwa sawa sawa na usemi huu Mwenyezi Mungu anasema ndani ya Qurani Tukufu:

قُلْ اِنْ كُنْتُمْ تُحِبُّوْنَ اللّٰهَ فَاتَّبِعُوْنِىْ يُحْبِبْكُمُ اللّٰهُ.....

“Ikiwa ninyi mwampenda Mwenyezi Mungu, Basi nifuateni, Mwenyezi
Mungu atawapendeni”(Aale Imran:3/32) kisha Anasema:

وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا اَشَدُّ حُبًّا لِّلّٰهِ۔

“Wale walioamini wanampenda Mwenyezi Mungu
zaidi.”(Albaqarah:2/166)
Mwenyezi Mungu amejaalia upendo kwa viumbe vyake vyote. Tunaweza kufahamu upendo wa mtu yeyote kutokana na sifa,tabia, khulka na mwenendo wake. Ama watu wa kidunia wanaipenda dunia
na watu wa Mungu wanampenda Mungu zaidi, na upendo wao kwa Mola wao unadhihirika katika matendo na mielekeo yao.

wa Qurani Tukufu - Mwenyezi Mungu anasema “Wale walioamini wanampenda Mwenyezi Mungu zaidi sana.”
Bila shaka Seyyidna Ahmad alitumia kila hatua ya Maisha yake katika
kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Akieneza ujumbe wa Mtume s.a.w na
kueleza mapenzi yake kwa ajili yake. Mtu huyu alitaabika mikononi
mwa watu wa taifa lake mwenyewe na wengine, kwa sababu ya
mapenzi yake kwa Mwenyezi Mungu, fikara yake kwa jina na heshima
ya Mtume s.a.w kila sehemu ya mwili wake akili na roho ilitolewa kwa
kumtumikia. Kwanza kabisa ningependa kueleza mfano wa utoto wake.

Siku moja Seyyidna Ahmad a.s alipokuwa anacheza na rafiki yake, Yeye
alimwambia aombe kwa ajili yake fadhili za Allah na msaada wake
kusimamisha sala kwa kadri apate mawasiliano na Allah.
Hebu! fikirini kidogo wakati wa utoto, ambapo mtoto hajui maana ya mapenzi ya Mungu na mawasiliano naye Seyyidna Ahmad a.s alikuwa anafikiri
kuhusu mawasiliano na Mwenyezi Mungu. Na wakati wa ujana wake ambapo mtu anakuwa na tamaa nyingi ya maendeleo na starehe za kidunia, yeye alikuwa anaishi hasa msikitini muda wake wote.
Siku moja rafiki wa baba mzazi wa Seyyidna Ahmad a.s aliyekuja kwa baadhi ya kazi zake. Yeye alimuuliza baba wa Seyyidna Ahmad a.s kwamba tunajua una watoto wawili, ila tunamuona mmoja tu, wa pili yuko wapi? Baba wa Seyyidna Ahmad a.s alisema, yeye hapendi kutoka nje sana anakaa ndani tu kama bi harusi. kama unapenda kukutana naye basi nenda msikitini utamuona pembeni, humo. Yeye daima
hushinda mlemle msikitini wala hana haja ya kazi nyingine ya kidunia.

Huu ni ushuhuda wa imani na mapenzi ya hali ya juu ya Seyyidna Ahmad a.s juu ya Mola wake, sawa na maneno ya Mtume s.a.w yasemayo(tafsiri ya kiarabu) Yaani yule mutu ambaye moyo wake
umefungamana na msikiti anakuwa chini ya rehma na msaada wa
Allah.
Pia Mwenyezi Mungu anaeleza ndani ya Qurani Tukufu kwamba (Tafsiri) Yaani anayestawisha misikiti ya Allah ni yeye tu amwaminiye
Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho.
Mzee mmoja wa kisinga singa akasimulia tukio moja huku akitokwa na
machozi, anasema hivi : safari moja baba yake Mirza sahib alinituma kumshawishi aonane na maafisa fulani kwa ajili ya kazi fulani kama vile
ukarani wa kodi, tulimkuta Mirza sahib katika faragha yake akijisomea,
tulimueleza madhumuni yetu kuwa, baba yako anakuuliza je, unataka
ufanye kazi serikalini ? Kwa hiyo jawabu lake lilikuwa.
« Nimechagua kumtumikia Bwana mmoja tu, Yeye ni Mola wangu, Ananitosheleza. »
Angalieni jinsi alivyomtanguliza Mola wake Juu ya vitu vyote, Je katika
hali hii akili ya Mtu yeyote inaweza kuwaza kwamba huyu alikuwa ni mtu mwongo ?

Itaendelea wiki ijayo

BISMILLAHI RAHMAAN RAHIIM
JAMIA AHMADIYYA WAADHIMISHA SIKU YA MWANA ALIYEAHIDIWA R.A

Kwa msaada maalum wa Mwenyezi Mungu na kwa baraka za khalifa wake mtukufu a.t.b.a ,wanachuo pamoja na wakufunzi wa chuo cha Jamia Ahmadiyya wamepata tena fursa ya kuadhimisha



Katika Jamia Ahmadiyya maadhimisho hayo yalifanyika siku ya Jumapili ya tarehe 20 February 2022.
moja ya siku muhimu kabisa katika jumuiya .Hiyo ni siku ya Musleh Mau’ud r.a ambayo huadhimishwa kila tarehe 20 ya Februari kila mwaka.
Hafla ilifanyika chini ya mwenyekiti ambaye pia ni mkuu wa chuo Maulana Sheikh Abid Mahmood Bhat sahib na ilianza majira ya saa 4:00 asubuhi kwa usomaji wa Qurani tukufu iliyosomwa na Ustadh Hussein.O.Mpenda na kufuatiwa na shairi la kiurdu lililosomwa kwa pamoja na Idd Tamimu na Swaleh Rajab.

Kisha ulifuata usomaji wa bishara kuu,ambaye ilisomwa na Ustaadh Rajab Luseza. Baada ya usomaji wa bishara kuu,ulifuata hotuba yenye maudhui isemayo,”Baadhi ya kazi alizofanya Hadhrat Muslih Mau’ud r.a’’..Hotba hiyo ilitolewa na ustadh Yakini Rajabu Sandari .Ustaadh alijitahidi kuwapitisha wasikilizaji katika matukio na kazi kemkem alizopata kufanya Mwana Aliyeahidiwa r.a ,hata hivyo mzungumzazji alikiri kuwa aliyoyawasilisha ni machache sana ukilinganisha na uhalisia wenyewe.Kwani sio rahisi kueleza japo kwa asilimia Hamsini ya kazi zote za mwana huyu.

Baada ya hotuba hiyo,ilifuata hotuba nyingine yenye maudhui isemayo,”Jinsi bishara ilivyotimia’’ ,hotuba hiyo ilitolewa na Mwalim Abdullah Rundo sahib ,mwalim sahib alifafanua hotuba yake kwa kurejea na kutaja matukio mbalimbali yanayothibitisha pasi na shaka yoyote juu ya kutimia bishara hiyo adhimu katika dhati ya Hadhrat Muslih Mau’ud r.a .
Akihitimisha hotuba yake mwalim sahib alitaja mambo kadhaa ya ghilba yalyofanywa na maadui wa dini tukufu ya islam ili kuwahadaa na hatimaye kuwatoa waislamu nje ya dini hii tukufu ya islam,na ukombozi ulioletwa na Hadhrat Muslih Mau’ud r.a kwa kutuletea wabashiri walonusuru Imani zetu.Baada ya hotuba hiyo,ilifuatwa na shairi la Kiswahili lililotungwa na kughaniwa na Ustaadh Juma Mwanyika.

Inaendelea Uk 4

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie
mapenziyamungu36@gmail.com